Ksh. 3,000

# UCHUNGUZI WA UOZO KATIKA MASHAIRI YA KHATIB NA KING'EI

NA

AYUB OYIMBA BARASA

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA

DESEMBA 2015

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine

Sahihi ……………………………………..Tarehe…11-11-2015……………………………

**BARASA O. AYUB**

**C50/CE/22590/2011**

Tasnifu hii imetolewa kwa chuo kikuu kwa idhini yetu kama wasimamizi

Sahihi ………………………………………………..Tarehe…11-11-2015……………………………

**DKT EDWIN MASINDE**

**IDARA YA KISWAHILI CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

Sahihi ……………………………………………………Tarehe…11/11/2015……………………………

**DKT JOSEPH MAITARIA**

**IDARA YA KISWAHILI CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**TABARUKU**

Naitabaruku kazi hii kwa marehemu babu Wambong'o, baba Musa, shangazi Msenya, baba Oyimba, pamoja na marehemu dada Makini, Christine, Bilhah, marehemu mke wangu Miriam miongoni mwa wengine. Mikononi mwa Mungu mnapumzika, moyoni mwangu mtaishi daima.

**SHUKRANI**

Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia Baraka zake hadi kutimia kwa kazi hii, ni kwa uwezo na neema zako tu ambapo kazi hii ilikamilika. Jehova utukuzwe daima.

Sina budi kuwatolea shukrani zisizo na kifani wasimamizi wangu Dkt Edwin Masinde na Dkt Joseph Maitaria kutokana na miongozo yenu ya busara pamoja na ushauri wa mara kwa mara nisingeweza kudhibiti vyema mawimbi makali ya bahari hii ya utafiti. Asanteni sana kwa kunivumilia kutoka mwanzo hadi mwisho.

Shukurani zangu ziwaendee wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili, kwa kuongoza na kujitolea kwao kulikofanikisha masomo yangu ya shahada ya uzamili hata lengo likatimia.

Nawashukuru wazazi wangu wapendwa Joseph Barasa na Jane Barasa kwa kugharamia masomo yangu, juhudi zenu za kunipa moyo kuendelea na masomo yangu hadi upeoni. Juhudi hizi ndizo misingi ya kazi hii. Mungu awabariki.

Michango waliyotoa ndugu zangu si ya kupuuzwa, ndugu Abraham, Phanice, John, Timothy, Elkah na Josephine. Kukamilika kwa kazi hii kulitegemea msaada wenu.

Muhimu sana nawashukuru wanangu Titus na Testim. Japo mamenu kafariki mkiwa wachanga, uvumilivu na ukakamavu wenu ulinipa nguvu ya kujisukuma na kutekeleza wajibu wangu kama ilivyonipasa. Mola awajalie maisha marefu yenye heri. Ninyi ndio mkongojo wangu wa baadaye.

Aidha, sitawasahau wazamili wenzangu tulioshikana mikono na kuvuka pamoja; Nasimiyu, Onyancha, Lucy, Brenda, Charity, Orina, Anyota, Mose. Kwa kunihimiza na kunifaa kwa vipakatalishi, vitabu na makala mengine. Mola awajalie mema.

Vilevile, namshukuru dada Rose kwa kukubali kunipigia chapa kazi hii.

Na wengine ambao sikuweza kuwataja hapa kwa majina. Nawahongera nyote mwenyezi Mungu awaepushe na maovu. AHSANTENI.

**IKISIRI**

Utafiti huu umeshughulikia uozo katika mashairi ya Khatib na King'ei kwa kuongozwa na nadharia ya kimtindo na maadili. Nadharia hizi zilifaa utafiti huu ikizingatiwa kwamba maudhui ya mtunzi na mtindo anaoutumia katika kutoa ujumbe wake ni vipengele vinavyotegemeana. Mtunzi hutunga kutokana na tajriba aliyopata katika mazingira yake na lugha ndiyo aitumiayo kueleza mambo mbalimbali ya jamii yake kwa njia ya kubuni.

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza imetupa mwelekeo wa utafiti, malengo ya utafiti na sababu za kuchagua mada. Hali kadhalika sura hii imeshughulikia misingi ya nadharia, upeo na mipaka na yaliyoandikwa kuhusu mada. Mwisho ni mbinu za utafiti na uchanganuzi wa data.

Sura ya pili imejadili mashairi yenye uozo wa kijamii kama vile ndoa, mapenzi, dini, utamaduni na falsafa kuhusu maisha. Tumeonyesha namna maudhui ya uozo kijamii yalivyojengwa kifani na mafunzo waliyotoa watunzi.

Sura ya tatu imejadili uchambuzi wa mashairi yenye maudhui ya uozo wa kisiasa. Tumeonyesha jinsi maudhui haya ya watunzi hawa yalivyosababisha uteuzi maalum wa lugha katika kuyaibusha.

Sura ya nne imejihusisha na uchambuzi wa mashairi yenye maudhui ya uozo wa kiuchumi. Katika sehemu hii, tumeonyesha jinsi mtindo maalum wa mwandishi unavyosadia kuibusha ujumbe wake na mafunzo wanayotoa waandishi kurekebisha hali ya uozo.

Sura ya tano ni hitimisho. Sura hii ni muhtasari wa matokeo ya utafiti wetu ambamo licha ya kueleza ugunduzi wa uchambuzi wetu tumetoa kauli yetu juu ya umuhimu wa utafiti wetu na maeneo ambayo yanastahili kufanyiwa utafiti zaidi hapo baadaye.

## YALIYOMO

**MADA**......................................................................i
**UNGAMO**......................................................................ii
**TABARUKU**......................................................................iii
**SHUKRANI**......................................................................iv
**IKISIRI**......................................................................v
**SURA YA KWANZA**......................................................................1
1.0 Utangulizi......................................................................1
1.1 Usuli wa Utafiti......................................................................1
1.2 Suala la Utafiti......................................................................4
1.3 Maswali ya Utafiti......................................................................5
1.4 Malengo ya Utafiti......................................................................5
1.5 Sababu ya Kuchagua Mada......................................................................5
1.6 Upeo na Mipaka......................................................................7
1.7 Yaliyoandikwa juu ya mada......................................................................9
1.8 Misingi ya Nadharia......................................................................13
1.8.1 Nadharia ya Kimtindo......................................................................13
1.8.2 Nadharia ya maadili......................................................................15
1.9Mbinu za Utafiti......................................................................17
1.9.1 Muundo wa Utafiti......................................................................17
1.9.2Mahali pa Utafiti......................................................................17
1.9.3 Sampuli Lengwa na Uteuzi wa Sampuli......................................................................17
1.9.4 Ukusanyaji wa data......................................................................18
1.9.5Uchanganuzi wa Data......................................................................18
1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti......................................................................18
**SURA YA PILI**......................................................................19
**UCHUNGUZI WA UOZO KIJAMII**......................................................................19
2.1Utangulizi......................................................................19
2.2 Uozo wa Kijamii......................................................................20
2.3. Kiishilio......................................................................37

**SURA YA TATU** .......... **39**
**UCHANGANUZI WA UOZO KISIASA** .......... **39**
3.1 Utangulizi .......... 39
3.2 Uozo wa Kisiasa .......... 39
3.3 Kiishilio .......... 55
**SURA YA NNE** .......... **56**
**UCHUNGUZI WA UOZO KIUCHUMI** .......... **56**
4.1 Utangulizi .......... 56
4.2 Uozo Kiuchumi .......... 56
4.3 Kiishilio .......... 67
**SURA YA TANO** .......... **69**
**MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI** .......... **69**
5.0 Utangulizi .......... 69
5.1 Muhtasari wa utafiti .......... 69
5.2 Matokeo ya utafiti .......... 71
5.3 Umuhimu wa matokeo ya utafiti .......... 78
5.4 Mapendekezo .......... 79
**MAREJELEO** .......... **80**
**FAHARASA** .......... **84**
Nyongesa I: Maelezo ya istilahi muhimu kama zilivyotumiwa katika tasnifu .......... 84
Nyongesa II: Mashairi Teule .......... 87

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia mambo ya kimsingi kuhusu utafiti. Tumeanza kwa kuangazia usuli wa utafiti, swala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti. Vilevile sababu za kuchagua mada na umuhimu wake, upeo wa utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na misingi ya nadharia. Aidha sura imehitimishwa kwa kufafanua mbinu zilizotumiwa katika utafiti, sampuli iliyoteuliwa,ukusanyaji wa data, mbinu za Uchanganuzi zilizotumiwa na matokeo yalivyowasilishwa.

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Utafiti huu umeshughulukia uozo katika mashairi ya Khatib na King'ei .Uozo katika muktadha huu ni ukiugaji wa maadili. Upotovu wa maadili katika jamii ni suala ibuka na nyeti.

Wafula na Njogu (2007),wanasema kuwa, fasihi ni usanii ambao hauwezi kujitenga na mazingira, msanii mara nyingi huzoa mawazo kutoka katika jamii yake. Lengo kuu la msanii ni kuarifu kuhusu ulimwengu na jamii kwa jumla. Wakati na nafasi kijamii ndio muhimu kwa msanii kwa jumla. Ni kutokana na haya tumeweza kuona namna wasanii Khatib na King'ei walivyoweza kutunga mashairi yanayogusia jinsi binadamu amegeuka kimaadili. Tumeweza kuangalia kazi zao kwa ambavyo waliweza kuangazia ugeukaji huu wa maadili unaoendelezwa na wanajamii.

Njogu na Chimerah (1999), wanasema kuwa fasihi inafungamanishwa na maisha ya binadamu. Kazi ya fasihi huenda isitoe habari za jumla bali kutupa miongozo ya ukweli kutokana na uteuzi na uwasilishaji wa tajirba maalum za wanajamii pia fasihi hutupa

nafasi ya kuhisi namna jamii ilivyokuwa, ilivyo na itakavyokuwa. Fasihi vilevile huweka wazi hali halisi ya jamii. Hii ni kwa sababu msanii ni zao la jamii na hujaribu kutuwasilishia matukio ya jamii katika uhalisi wake. Kila fasihi huwa ni zao halisi la jamii na huonyesha kuwepo kwa jamii hiyo kijamii, kisiasa na hata kiuchumi. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yanaweza kubainishwa kupitia fasihi. Isitoshe, itikadi za jamii fulani zinaweza kujulikana kupitia fasihi. Kadri tunavyofahamu fasihi ya kundi fulani au jamii fulani ndivyo tunavyofahamu kwa kiasi kikubwa mambo yanayofanya jamii au kundi fulani kuwa jinsi ilivyo. Waandishi wa kazi ya fasihi wametumia mbinu za sanaa kama vile kupiga chuku, kejeli, istiari na mbinu nyinginezo ili kuonyesha uhalisi wa kijamii kwa njia ya ubunifu. Ni muhimu kuchunguza kazi ya fasihi kwa umakini iIi kudhihirisha jinsi waandishi wetu wa mashairi waIivyochora ukweli kuhusu uozo wa jamii.

Chiraghdin(1986) katika Utangulizi wa *Malenga wa Mrima* anasema kuwa mshairi wa Kiswahili ni mwakilishi wa umma. Anaendelea kusema kwamba, jambo lisemwalo wakati huo haliwi lake binafsi bali hulisemea umma uliomzingira ikiwa ni kuonya, kuliwaza, kuwapongeza, kuwahimiza wanajamii. Aidha, lile alilonalo huwa ni jambo ambalo huweza kumpata mcha yeyote kwa wakati wowote. Ndiposa mtu akilisoma shairi anaweza kuyapima yaliyomo kwa mizani ya jinsi yalivyomchoma wakati wake. Hivyo, washairi Khatib na Kinge'i wametufichulia maadili potovu ya binadamu.

Mzenge na Said (1993) wanasema kuwa, mshairi wa Kiswahili ana sababu nyingi zinazomfanya atunge mashairi. Ni mtu aliye macho daima. Ni nadra kumwona amenyamaa panapotukia jambo fulani. Akiona jamii au taifa lake linaelekea kombo

anatahadharisha na kulizindua. Hupenda kukashifu uongozi wa nchi yake. Washairi hufanya hivi kwa kutumia lugha ya kimafumbo na mnato wa hali wa juu. Kwa jumla lengo muhimu la shairi ni kuhifadhi utamaduni na historia ya jamii.

Washairi wana nafasi mbalimbali katika jamii kama vile kukashifu uovu katika jamii. Wametambua kuwa maisha si jana na leo tu, bali pia kuna kesho ambayo ifanyiwe matayarisho yake leo. Wao kwanza hupiga mbizi na kuangazia tulikotoka na kuelewa barabara kilicho sababisha hali tulio nayo sasa. Hii imetusaidia kuelewa kuwa washairi Khatib na Kinge'i wameangazia matukio ya uovu katika jamii. Waligusia na kukashifu tabia za upotovu wa maadili kijamii, kisiasa na hata kiuchumi katika mashairi yao.

Gibbe (1979), anasema fasihi ina majukumu ya kuelimisha na kusisimua. Katika kuelimisha ina jukumu la kuichora jamii kama ilivyo. Fasihi hujaribu kuyamulika matatizo yanayoizonga na kuinyonga jamii. Fasihi inapaswa kuwafungua watu macho iufichue uchafu uliosakini katika jamii. Wakandamizwaji wafichuliwe, wakandamizwao wapewe mwongozo sahihi waitambue hali yao dhaifu. Zaidi ni kuwa ili fasihi iwe na manufaa katika jamii pia ni chombo cha kuilekeza jamii hiyo. Ni muhimu iwe na jukumu la kutekeleza, kuichambua, kuikosoa na kuingoza jamii katika lengo lake la kupindua unyonge na uchafu uliosakini katika jamii hiyo.

Unacharsky (1973), anasema ni muhimu fasihi ipongeze watu kwa mchango wanaofanya katika jamii. Isiogope kuwahukumu wanaopotosha jamii. Ni kutokana na hayo utafiti huu umefanywa iIi kuangazia uozo wa binadamu ulivyosawiriwa katika mashairi ya uozo.

### 1.2 Suala la Utafiti

Uchunguzi huu ulishughulikia uozo katika mashairi ya Khatib na King'ei. Msanii anaweza kuangazia suala ibuka katika jamii kwa lengo la kuarifu au kutahadharisha. Upotovu wa maadili katika jamii ni suala ibuka na nyeti. Kwa hivyo, ni muhimu kuchunguza jambo hili katika jamii ya sasa ili tulielewe nje na ndani.Vilevile,ni muhimu tuone athari zake na jinsi ya kukabiliana nazo. Ni kutokana na haya ndipo utafiti umeonyesha jinsi upotovu wa maadili unavyoweza kusomwa katika mashairi ya Khatib na King'ei. Utafiti umeainisha na kuchanganua mashairi yalivyomchora binadamu kisiasa, kiuchumi na kijamii kama kiumbe aliyepotoka kimaadili.

Msokile(1986)anasema kwamba, washairi wana nafasi muhimu katika jamii wanamoishi kama vile kukashifu uovu, huzindua, kuelekeza, kutahadharisha na kuelimisha. pia msanii ana dhima ya kuelimisha jamii kuhusu yanayoendelea na kumulika matarajio ya wanajamii, kukashifu maovu yaliyo katika wanajamii na kutoa mwelekeo unaofaa. Aidha, mtunzi huathirika na mazingira anamoishi na athari anayopata humpa msukumo wa kutunga kuhusu jambo linalomkera.pia kuna uhusiano mkubwa kati ya matukio na mfumo mzima wa maisha. Hivyo dhamira ya mtunzi huathiriwa na mazingira anamoishi na humpa msukumo wa kutunga kazi yake ili apate kutoa msimamo wake kuhusu maswala mbalimbali ya kijamii. Vilevile, mtunzi akiwa kama mwalimu daima huwa anashughulikia maswala yanayoathiri jamii yake. Huwa ni nadra kumpata amenyamaza na huku jamii yake inaathirika. Kadri mtafiti ajuavyo utafiti kuhusu kazi teule ilikuwa haichafanywa na mtafiti mwingine.

### 1.3 Maswali ya Utafiti.

Utafiti huu umeongozwa na maswali matano muhimu:

a. Ni uozo gani unajitokeza katika mashairi ya Khatib na King'ei?

b. Ni kwa namna gani uozo umeendelezwa katika jamii?

c. Ni kina nani wamehusika katika kuendeleza uozo katika jamii?

d. Je,mtunzi ana jukumu lipi la kuirekebisha jamii yake kimaadili?

e. Watunzi wa mashairi walishughulikia vipi suala la uozo katika mashairi yao?

### 1.4 Malengo ya Utafiti.

Malengo ya utafiti huu yalikuwa yafuatayo;

1. Kubainisha uozo unaojitokeza katika mashairi ya Khatib na King'ei.
2. Kubainisha namna uozo unavyoendelezwa katikajamii.
3. Kuonyesha wanaohusika katika kuendeleza uozo huo.
4. Kubainisha nafasi ya mtunzi katika kuirekebisha jamii yake kimaadili.
5. Kueleza namna watunzi walivyoshughulikia suala la uozo katika mashairi yao.

### 1.5 Sababu ya Kuchagua Mada

Njogu na Chimerah (1999) Wanasema kwamba, fani na maudhui ni vipengele vinavyotegemeana na kuathiriana katika kazi moja kiasi kwamba mtunzi anapofikiri kuhusu swala la kushughulikia katika shairi Vilevile,hufikiria lugha atakayotumia ili kuibua ujumbe wake vizuri.Utanzu wa ushairi katika siku za hivi karibuni umekuwa muhimu katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya jamii katika nyanja mbalimbali. Mashairi yamekuwa fimbo muhimu ya kuirekebisha, kuiongoza, kuelimishana kuzindua jamii hasa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kama sehemu ya fasihi, ushairi una lengo la kuwasilisha hisi za ndani za mtunzi. Ushairi huambatana na shughuli za kila

siku katika jamii. Ni kwa sababu hii ambapo ushairi unahitaji kufanyiwa utafiti zaidi kwa upande wa uozo katika jamii na kufafanuliwa ili kueleweka na wengi.

Khatib na King'ei ni waandishi na watunzi wa mashairi ya kisasa.pia wanashughulikia maswali yanayokumba jamii ya sasa. Kwa hivyo, ilikuwa muhimu kuchunguza namna walivyoshughulikia swala la uozo katika jamii ya sasa.

Fasihi ina uhuru kuonyesha kasoro zilizomo katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Fasihi ni taaluma pana na nyumbufu ya kuweza kuwakosoa wanajamii na kuwaelekeza kwa njia faafu.

Kulingana na Ngure (2003), wasanii huonyesha ustadi wao katika kutumia maneno kisanaa ili kuwasilisha ujumbe wao kwa jamii inayohusika. Utafiti umechunguza jinsi washairi walivyotumia ubunifu katika kuwakosoa wanajamii kutokana na mienendo inayoashiria utovu wa maadili

Sababu nyingine ya kulichagua somo hili, ilitokana na imani yetu kwamba kuna uhusiano mkubwa baina ya sanaa na matukio ya kijamii. Kwanza msanii ni mmoja katika jamii ya binadamu mwenye ubunifu na uwezo wa kufurahia ubunifu huo. Hawezi kujitenga na matukio ya jamii yake. kwa sababu ana maslahi katika jamii hiyo. Pia, kazi yake ni kiungo chake na jamii anayoitungia. Msanii hutarajia kwamba atakuwa pamoja na hadhira yake kihisia na kwa hivyo kujitahidi kuufanya umbuji wake uziteke hisi za hadhira yake. vilevile, kazi ya sanaa ina taathira kwa wanajamii. Hutilia nguvu au kudhoofisha mawazo yao, matarajio yao na hofu zao. Jamii ndiyo impayo ilhamu msanii akasanifu ikiwa anaonyesha mguso iupatao kutokana na sanaa yake. (Vasquez 1973).

Utafiti huu ulitokana na sababu kwamba ungewafaa wanafunzi, walimu, wahakiki, watunzi wa mashairi na hata wakuzi wa mitaala. kwa vile wataelewa namna ya kuhakiki mashairi kwa upande wa lugha inayotumiwa na dhamira ya watunzi.

**1.6 Upeo na Mipaka.**

Kuna tanzu nyingi za fasihi ya Kiswahili lakini utafiti huu ulizingatia utanzu wa ushairi ambao ni mkongwe zaidi kuliko tanzu nyinginezo. Una historia ndefu na umetumikia jamii kwa njia tofautitofauti.

Utafiti huu tumezichunguza diwani za Khatib na Kinge'i ambazo zina maudhui maalum ukiugaji wa maadili. Kazi hii vilevile imeshughulikia maudhui na lugha ilivyotumiwa kuwasilisha ujumbe.

Ingawaje wasanii hawa wameandika hadithi fupi, fasihi simulizi, tamthilia na ushairi. Utafiti wetu umejikita katika kuzitalii diwani zao mbili (*Wasakatonge* na *Miale ya Uzalendo*), kwa upande mwingine yaliyomo na mbinu anazotumia msanii huchangiana na kujaziana katika kuwasilisha ujumbe wake. Tumetaja mbinu zilizotumiwa ili kufafanua ujumbe unaowasilishwa kupitia kwa matumizi ya mbinu hiyo kwa vile hatuwezi kuelewa maudhui bila kuhusisha mbinu alizotumia mwandishi. Utafiti huu ulizingatia mbinu kama vile jazanda, kejeli, taswira, tashbihi, tashhisi, maswali ya balagha, semi, methali na takriri.

Tumeonyesha kuwa lengo letu katika kuyachambua maudhui ni kuweza kuangazia jamii ilivyo kutokana na maudhui hayo. Katika hatua hii tumejifunga katika utalii wa uozo jinsi ulivyojitokeza katika maudhui ya waandishi.

Kuna watunzi wengi wa mashairi lakini utafiti huu umeshughulikia ushairi wa Khatib na King'ei. Tulimchagua Khatib kwa ambavyo ni mtunzi kutoka Tanzania na King'ei kutoka nchini Kenya. Kwa kuwachagua watunzi hawa kutoka mazingira tofauti ili kubaini jinsi mazingira tofauti yanavyosawiri swala moja.

Kuna maswala mbalimbali ambayo yanaweza kushughulikiwa katika uhakiki wa ushairi lakini katika muktadha wa utafiti huu umezingatia tu uozo katika jamii kwa ambavyo hili ni swala nyeti ambalo linaathiri jamii ya sasa na ya baadaye na ambalo lilifaa kushughulikiwa ili mikakati mwafaka iweze kuwekwa ili kukabiliana nalo.

Utafiti huu umeshughulikia mashairi ishirini na moja kutoka diwani mbili za washairi wawili. Diwani hizo ni *Miale ya Uzalendo*(2000) ya King'ei na *Wasakatonge* (2003)ya Khatib. Kazi hii imejikita katika uchambuzi wa uozo katika baadhi ya mashairi yaliyotungwa na Khatib na King'ei katika tungo zao.

Tumeyagawanya mashairi hayo katika maudhui ya kisiasa, kiuchumi na masuala mengine ya kijamii. Mashairi yaliyoshughulikiwa ni kama yafuatayo.

**Siasa**

| | |
|---|---|
| Kinyume cha katiba - Miale ya Uzalendo | uk. 82 |
| Wafrika unganeni | uk. 13 |
| Uzuzu | uk. 120 |
| Ndumakuwili | uk. 155 |
| Madikteta - wasakatonge | uk. 21 |
| Miamba | uk. 29 |

| | |
|---|---|
| Hatukubali | uk. 30 |
| Wafadhiliwa | uk.38 |
| Nahodha | uk.41 |

**Uchumi.**

| | |
|---|---|
| Hatuna kauli | uk.8 |
| Walala hoi | uk.36 |
| Klabu | uk.50 |
| Mbona matatu zaua? - miale ya Uzalendo | uk.157 |
| Acheni milimbiko | uk.25 |

**Maswala mengine ya kijamii.**

| | |
|---|---|
| Tohara – wasakatonge | uk.2 |
| Afrika | uk. 6 |
| Unyama | uk. 47 |
| Mbona mwateta? - miale ya Uzalendo | uk. 23 |
| Uvundo | uk.77 |
| Wake wenza | uk. 101 |
| Afrika yaugua | uk. 170 |

## 1.7 Yaliyoandikwa juu ya mada.

King'ei na Kemoli (2011), wanasema kwamba ushairi ni chombo mwafaka kinachomwezesha mwandishi kuufumbata upana na urefu ya maisha katika maneno teule machache yaliyifinyagwa kisanaa. Kazi ya washairi hawa wawili imetufaidisha kwa

sababu wametuonyesha hatua za kuzingatia ili kudondoa maudhui ya mshairi hasa maudhui ya uozo.

Babusa (2005), alichunguza vigezo mbadala kuainisha mashairi ya Kiswahili ili kuepuka mgogoro kati ya wanajadi na wanausasa. Baadhi ya vigezo alivyozingatia ni maudhui, fani, idadi ya mishororo miongoni mwa vigezo vingine.Tofauti kati ya kazi hizi mbili ni kuwa utafiti wa Babusa ulizingatia vigezo vya uainishaji wa ushairi ilhali utafiti huu umejikita katika upotovu wa maadili kwa kina zaidi. Aidha, misingi ya kinadharia ni tofauti. Babusa alitumia nadharia ya tanzu ilhali utafiti huu umezingatia nadharia ya kimtindo na maadili.

Wanyama (2006), alichunguza maudhui ya mtindo katika utendi wa Wabukusu wa "khuswala kumuse". Tofauti kati ya kazi hizi mbili ni kuwa Wanyama alishughulikia mtindo na maudhui kwa ujumla ambapo utafiti huu umezingatia kitengo kimoja tu cha maudhui - upotovu wa maadili na kuzama zaidi. Pia Wanyama alishughulikia utendi ambapo utafiti huu utazingatia mashairi kadhaa yaliyoteuliwa.

Muhammed Seif (1985), *Mulika,* anajadili maudhui ayachotayo mtunzi kutoka mazingira yake anasema, fasihi ni sanaa itumiayo maneno katika kuyaeleza na kuyahakiki maisha na mazingira ya jamii ni zao la jamii, huchota maudhui yake katika harakati za kimaisha huku vionjo na matamshi ya watu wa jamii hiyo katika muhula maalum. Uzito wa maudhui na ukuu wake hutegemea mwandishi jinsi anavyojadili maisha. Ukamilifu wa kazi kifasihi hutegemea mwandishi jinsi anavyojadili mazingira na maumbile ya jamii alimoibukia. Kazi hii itatufaa kwa ambavyo uozo wa binadamu umesawiriwa katika mashairi kwa madhumuni ya kuadilisha.

Sengo(1973), anatueleza dhima kubwa ya fasihi ni uteuzi na ufasiri wa amali za jamii ambazo ni tamaduni, mila, dini, siasa na uchumi. Fasihi pia hushughulikia masuala mbalimbali yanayoikumba jamii. Mojawapo ikiwa upotovu wa maadili. Watunzi wetu Khatib na King'ei wameweza kuangazia uozo wa binadamu kisiasa,kiuchumi na kijamii katika mashairi yao.

Chacha (1987), ameshughulikia maana na ufasiri wa mashairi ya Kiswahili. Yeye alichunguza madadiliko ya kijamii na kiuchumi ya waswahili wa mvita yalivyoathiri matumizi ya jazanda katika mashairi. Kazi hii ni tofauti na yetu kwa ambavyo utafiti wetu umeangazia namna mashairi ya Muhammed Seif na Kitula King'ei yalivyomchora binadamu kama kiumbe aliyepotoka kimaadili.

Kibwana (1996) anasema kiongozi yeyote anastahili kuwa na maadili ya juu na ya kuheshimiwa, maovu yanayokashifiwa ni ufisadi katika kutumia raslmali ya nchi, ubaguzi kutokana na ukabila, uongozi wa mapendeleo na magendo. Kazi hii ni muhimu kwetu kwa sababu imetuongoza katika baadhi ya maovu yanayotekelezwa na viongozi. Kazi hii ni tofauti na yetu kwa sababu yeye alikuwa akiangazia katiba ya chama cha DP nasi tumeangazia mashairi ya Muhammed na Kitula. Mlacha (1984),anapozungumzia wahusika katika riwaya za Kiswahili Tanzania. Katika utangulizi anasema kuwa, dhamira kuu ya mwanafasihi katika tanzu yeyote ya fasihi ambayo ataishughulikia huwa hasa ni kuyatumia maandishi au masimilizi kwa ajili ya kuwalea na kuwakuza watu wake wenye maadili na falsafa njema.Fasihi yetu licha ya kuonyesha falsafa potovu waliyo nayo baadhi ya wandishi wetu hawajaweza bado kuyachambua na hata kuyaelewa vizuri.

Hivyo basi utafiti wetu utafaidi jamii kwa ambavyo unaendelea kutafiti dhima ya msanii hasa katika kuangazia maovu ya binadamu.

Mnyampala (1980), anasema mashairi yana sifa iliyobora ulimwenguni na mafunzo yenye uadilifu na mazingira ya dunia yalivyo. Kauli hii imetusaidia pamoja na diwani na Muhammed Seifna kitula King'ei kuelewa maadili yanayotarajiwa kutoka kwa binadamu.

Masinde (1992) anasema mazingira ya mwandishi katika ujumla huathiri uteuzi wake wa dhamira na mtindo. Yeye alishughulikia ushairi huru pekee. Anasema dhamira ya mwandishi hutokana na mazingira yake ambayo humpa msukumo wa kutunga shairi. Kwamba ni tokeo la mwingiliano kati ya mtu na mazingira yake kuonyesha namna anavyoyapa fasiri yake. Kazi yake ni tafauti na yetu kwa namna ambavyo alishughulikia mashairi huru pekee ilhali kazi yetu imeshughulikia mashairi huru na ya arudhi. Aidha kazi hii imetufaa kwa ambavyo mazingira yanayomchochea Muhammed Seif na Kitula Kinge'i kuandika tungo zao zinazoonyesha jinsi jamii imepotoka kimaadili.

Masinde(2003), alipendekeza katika kazi yake kuwa ushairi uainishwe kwa misingi ya vipindi mbalimbali hasa vigezo vya maudhui, mtindo, muundo na utenda kazi bali sio arudhi. Kazi hii imetufaa katika uchambuzi tulipokuwa tunaainisha mashairi ya upotovu wa maadili yalivyotungwa na watunzi wetu

Samora (1977), anasema ni lazima tufahamu kuwa ujinga wa mtu mmoja ni udhaifu wa jamii nzima na huathiri kazi ya kila mmoja. Wanaokosolewa wasione haya, wala chuki bali wafurahi kuwa adui amegunduliwa. Makosa ya mtu mmoja huifanya kazi ya kila mtu kuwa nzito zaidi, huhatarisha malengo ya jamii na kuidhaifisha jamii nzima. Anaendelea

kusema kwamba waandishi wasione haya kuyataja makosa yanayofanyika katika jamii. Amesisitiza kuwa, makosa yafanywayo na mtu binafsi au jamii nzima yanapaswa kuwa mwongozo wetu wa baadaye. Kwa hivyo, ni muhimu sana kuangazia maadili na mienendo ya binadamu. Kazi hii ilituelekeza katika kujua maadili yanayostahili kuangaziwa na watunzi kama tulivyotathmini kwa kutumia diwani za Muhammed Seifna Kitula King'ei.

## 1.8 Misingi ya Nadharia.

### 1.8.1 Nadharia ya Kimtindo

Nadharia hii inaeleza kwamba kazi ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha. Kwa hivyo jinsi mtunzi atumiavyo lugha husaidia kutoa ujumbe wake kwa wasomaji au wasikilizaji. Hivyo, lugha ndicho chombo muhimu cha mawasiliano katika jamii zote za wanadamu. Chambilecho Leech (1969: 4). Kazi ya fasihi haiwezi kueleweka vizuri bila kuwa na ufahamu mzuri wa lugha ambayo hutumiwa kuieleza. Ni muhimu kuelewa uhusiano ulioko kati ya lugha na ushairi na ujumbe wa mwandishi.

Mwasisi wa nadharia hii (Buffon 1930) anadai kwamba mtindo ni mtu mwenyewe. Yaani jinsi mtu anavyotumia lugha kupitisha ujumbe wake. Buffon anaendelea kudai kwamba kazi ya fasihi hudumu kupitia mtindo wake na mtindo huu ni mtu mwenyewe.

Naye Ngare (1981) anafafanua mtindo kuwa ni namna ya kujieleza kwa kutumia lugha yaani ni namna mtunzi anavyowasilisha ujumbe wake. Nadharia ya kimtindo inaeleza kwamba kazi ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha. Kwa hivyo,jinsi msanii atumiavyo lugha husadia kutoa ujumbe wake kwa wasomaji. Hivyo lugha ndicho chombo muhimu cha mawasiliano katikajamii zote za ulimwengu.

Wanamtindo wanasisitiza umuhimu wa lugha kama chombo tekelezi kinachosaidia katika kuelewa ujumbe au maudhui yaliyokusudiwa na bila lugha hakuna fasihi. Aidha, Wanamtindo hawa wanaeleza kwamba vipengele vya kiisimu hutumika katika kueleza jinsi ambavyo lugha hutumika katika kazi ya fasihi. Kutokana na mtindo wa kazi ya fasihi inakuwa vigumu kubadili sentensi au hata neno katika kazi hiyo bila kubadili mtindo wenyewe.

Leech anaeleza kuwa mashairi hutumia lugha kiajabu na athari za ujumi haziwezi kutenganishwa na matumizi ya lugha kisanaa. Kuyashadidia maelezo haya Senkoro (19882) anaeleza kwamba ushairi ni utanzu wa fasihi unaotumia mpangilio wa lugha ya mkato, ya picha na yenye mapigo mahususi katika kutoa maudhui. Kwa hivyo vigezo vinavyotumiwa kuchambua na kubainisha ushairi ni umbo lake pamoja na matumizi ya lugha. Aendelea kueleza kuwa ushairi hutumia lugha ya mkato yenye kueleza maudhui yake kimhutasari na aghalabu huyaficha maudhui hayo ndani ya taswira na ishara. Hivyo, ushairi huwa hutumii lugha ya kinathari, ya mjazo na mtiririko.

Lodge (1988) anasema kuwa mtindo ni jinsi ya kujieleza ule upekee wa mwandishi wa kueleza kisanaa mambo ya kawaida. Ndiyo sababu uteuzi wa tamathali za usemi na msamiati hutegemea mtindo wa msanii binafsi. Kulingana na maelezo ya mwandishi huyu ni wazi kwamba mtindo wa msanii mmoja utakuwa tofauti na msanii mwingine ndiyo sababu tunaweza kufanya utafiti wa aina moja lakini kazi za waandishi mbalimbali

Kulinga na Leech (1969) kazi ya fasihi hukusudia kuwasilisha hisi au tajriba fulani kwa msomaji au msikilizaji. Aeleza kuwa nadharia hii ina vigezo vinavyotumiwa kuchambua

kazi za kisanaa kwa kuangalia mitindo ya mwandishi.Mihimili yake iliyotumiwa katika utafiti huu ni;

a. Maudhui na dhamira hushughulikia maoni au falsafa ya mtunzi juu ya jamii anayoizungumzia.Mhimili huu umetusaidia kuonyesha dhamira za watunzi pamoja na kueleza jinsi maudhui hayo ya upotofu wa maadili yanavyowiana na matumizi ya lugha.

b. Muundo wa kazi za kubuni ndio hutumiwa na msanii kutoa ujumbe wake. Huu ni mkondo anaofuata msanii katika kuifuma kazi yake.kwa mfano, jinsi mtunzi alivyounganisha tukiomoja na lingine, wazo moja na lingine au ubeti na ubeti ama mstari wa ubeti na mwingine. Mhimili huu umetusadia kuelewa namna watunzi walivyowasilisha ujumbe kuhusu mienendo inayoashiria uozo katika jamii.Hivyo ulituwezesha kutathmini nafasi ya watunzi katika kuirekebisha jamii.

### 1.8.2 Nadharia ya maadili

Nadharia hii inamhusisha mwanafalsafa na mhakiki ya Kiyunani aitwaye Plato katika andiko lake *The Republic* (443) Plato anasema kuwa kuishi kwa uadilifu ni sawa na kuishi kwa raha. Plato anamtumia Socrates kuonyesha umuhimu wa uadilifu. Kupitia mhusika Socrates, anasema kuwa ni utovu wa haki na maadili kuiba mahekaluni, kuwasaliti marafiki, kuvunja kiapo, kuzini na kuwadhulumu wanajamii wengine.

Tolstoy (1960) anaeleza sanaa kama uwezo wa kusimulia mambo yayohusiana na maadili ya jamii. Anaendelea kusema kuwa ujumi na uzuri wote wa sanaa hutegemea maadili ambayo hupitishwa kwa wanajamii. Pia sanaa nzuri ni ile ambayo inaweza

kupitisha ujumbe kwa watu wengi na ieleweke na kila mtu wanaitifaki wa nadharia hii wanadai kuwa fasihi inaeleweka vyema inapohusika na mazingira ya kijamii.

Wahakiki wa Kimagharibi wanaunga mkono nadharia hii kwa kusema msanii huwa na fahamu na huathiriwa na jamii yake. Isitoshe, yeye huandikia yale yanayoipa mwongozo mzuri maisha ya binadamu. Waasisi wa nadharia hii ya maadili wanasema kuwa ili binadamu awe kamili lazima awe mwadilifu, mwenye kiasi na mpenda haki. Haya ni kwa mujibu wa *Stanford Encyclopedia of Philosophy (2004).* Ni kutokana na maelezo haya, ndipo tumeweza kutathmini mashairi ya uadilifu ya khatib na king'ei kuangazia mihimili ifuatayo:

1. Umuhimu wa uadilifu ni kutovunja kiapo au kusaliti marafiki. Mhimili huu umetuwezesha kuonyesha wanaohusika katika ukiugaji wa maaadili kijamii, kisiasa na kiuchumi.
2. Sanaa ina uwezo wa kusimulia mambo yanayohusiana na maadili.Mhimili huu umetuwezesha kuonyesha namna uozo umeendelezwa katika jamii.
3. Msanii huwa na dhamira ya kuandika yale yanayojenga jamii kimaadili. Mhimili huu umetusaidia kubainisha majukumu ya mtunzi katika kuirekebisha jamii yake kimaadili.
4. Fasihi inaeleweka vyema inapohusishwa na mazingira ya kijamii. Mhimili huu umetuwezesha kuonyesha uozo unaojitokeza katika mashairi ya Khatib na King'ei.

## 1.9Mbinu za Utafiti.

### 1.9.1 Muundo wa Utafiti.

Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo, umetekemea mbinu ya kimaelezo katika kueleza na kutoa mifano mwafaka ya jinsi uozo wa kijamii, kisiasa na kiuchumi ulivyodhihirika katika diwani teule.

### 1.9.2Mahali pa Utafiti.

Utafiti umefanywa maktabani. Mtafiti amepitia vitabu, majarida na magazeti yanayozungumzia upotovu wa maadili.

Tafiti za awali zimesomwa ili kuelewa nadharia, mbinu za kukusanya data, uwasilishaji, uchanganuzi na matokeo ya utafiti. *Diwani za Wasakatonge* na *Miale ya Uzalendo* zimesomwa ilikubaini jinsi waandishi walivyoangazia maudhui ya uozo hasa kiuchumi, kijamii na kisiasa.

### 1.9.3 Sampuli Lengwa na Uteuzi wa Sampuli.

Sampuli lengwa katika utafiti huu ilikuwa diwani teule za Khatib na King'ei zilizoshughulikia uozo katika jamii.

Utafiti huu umetumia mbinu kusudio katika usampulishaji wake wa mashairi, mashairi teule yenye data ambayo imetimiza malengo ya utafiti huu ndiyo yameteuliwa kimakusudi. Kwa hivyo, kazi za washairi (Khatib na King'ei) zimeteuliwa kimakusudi kwa sababu waliandika kazi zao katika kipindi mahususi hasa katika karne ya ishirini na moja kwa misingi ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Aidha, mashairi ya uozo yameteuliwa kutokana na sababu kuwa suala la uozo limepitia changamoto katika jamii nyakati zote.

### 1.9.4 Ukusanyaji wa data

Njia kuu iliyotumiwa kukusanya data ilikuwa usomaji wa mashairi teule.Katikakufanya hivyo,mtafiti alinukuu sehemu zenye kuashiria uozo na utovu wa maadili. pia alinukuu wale walioendesha uozo katika jamii.Vilevile, alinukuu sehemu zilizodhihirisha namna uozo ulivyoendeshwa.pia mtafiti alinukuu sehemu za mashairi yaliyokuwa na vipengele vilivyoashiria uozo katika jamii.

### 1.9.5Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi umeongozwa na maswali na malengo ya utafiti kuonyesha namna mashairi ya Khatib na King'ei yamesawiri uozo ulivyosakini katika jamii na unavyoiathiri, kueleza jinsi uozo huo unaendelezwa katika jamii,namna uozo ulivyosawiriwa,kubainisha wanaohusika katika kundeleza uozo huo na kisha kuangazia jukumu la mwanasanaa katika kuirekebisha jamii yake kimaadili.

Tumeongozwa pia na mihimili ya nadharia ya kimtindo na nadharia ya maadili, Tumezingatia mashairi ya uozo wa kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kwa kuangalia yalivyoisawiri jamii.

### 1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo haya yalihusu uozo unaojitokeza katika mashairi teule, uozo huo unavyoendelezwa, wanaoendeleza uozo huo, namna watunzi walivyosawiri uozo katika mashairi yao na nafasi ya mtunzi katika kuirekebisha jamii yake kimaadili. Pia mifano ilitolewa katika sehemu za mashairi zilizozingatia vipengele hivyo.Vilevile, mifano mahususi ilitolewa kueleza na kufafanua uozo katika jamii kwa mujibu wa malengo ya utafiti.

## SURA YA PILI

## UCHUNGUZI WA UOZO KIJAMII

### 2.1Utangulizi

Katika sura ya kwanza, tulijadili mwelekeo wa utafiti wetu. Sura hiyo ilijadili mambo ya kimsingi kuhusiana na utafiti. Haya ni pamoja na ufafanuzi wa istilahi muhimu, usuli wa mada, swala la utafiti, malengo ya utafiti na sababu ya kuchagua mada. Mengine ambayo yalishughulikiwa ni pamoja na misingi ya nadharia, upeo na mipaka na yaliyoandikwa kuhusu mada. Hatimaye sura ilishughulikia mbinu za utafiti, mbinu ya kukusanya data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo. Sura hii tumewasilisha mashairi ya uozo kijamii.

Tumeshughulikia mashairi haya kwa lengo la kubainisha madhara yake kwa wanajamii. Aidha, tulionyesha namna uozo wa kijamii umeendelezwa katika jamii kwa mujibu wa mashairi ya King'ei na Khatib. Isitoshe, katika mashairi ya uozo kijamii, tumebainisha wanaohusika katika kuendeleza uozo huo na kudhihirisha majukumu ya wasanii wetu katika kuirekebisha jamii kimaadili. Katika kufanya hivi, tumeongozwa na nadharia ya maadili isemayo kwamba, fasihi hueleweka vyema inapohusishwa na mazingira ya kijamii. Aidha, tumeonyesha namna maudhui hayo yalivyojengwa kifani kwa kuongozwa na nadharia ya kimtindo isemayo kwamba huwezi kutenganisha ujumbe wa mtunzi na namna anavyoushughulikia ujumbe huo.

## 2.2 Uozo wa Kijamii

Miongoni mwa majukumu ya fasihi ikiwemo ushairi ni kukosoa jamii kutokana na mawazo bahali ambayo yanaweza kuipotosha. Katika kitengo hiki, tumeshughulikia mashairi yanayoonyesha matukio yanayojiri na kuathiri jamii.

Katika shairi "Afrika Yaugua" uk170 lililo katika diwani ya *Miale yaUzalendo,* King'ei anayamulika maovu yanayojiri katika bara la Afrika na kuliona kama bara linaloteseka "Kwa madhila kaka kaka" kwa ambavyo uovu huu umeenea na hauwachi kulitesa bara hili. Katika ubeti wa pili anatumia taswira ya vita vya ukombozi wa bara Afrika, kwa ambavyo penye vita huwa na maumivu,mahangaiko nahata vifo ndipo anasema "Roho nyingi kututoka," kwa maana ya vifo vinavyotokana na "ukombozi kuuzaka" kwa maana ya kuutafuta ukombozi kutokana na madhila yanayolikumba bara la Afrika. Ili kupata ukombozi huu mtunzi anasema kuwa "Zimetimu hekaheka"kwa maana ya ghasia na fujo zinazokumbakila pembe ya bara la Afrika. Vita hivi ni vya waafrika wenyewe kwa wenyewe kwa kutumia zana za kivita. Mtunzi anasema:

sasa vita vimefuka.
kila pembe Afrika.
kote bunduki zalika
kuitweza Afrika.

Mtunzi anasema "Sasa vita vimefuka" kwa maana ya vita vimeenea katika kila sehemu ya bara la Afrika na kila uendapo "bunduki zalika" kwa maana milio ya risasi yasikika kwa hivyo bunduki zinapolika ni ishara ya maafa ya maangamizi ya waafrika kila pembe na vivyo hivyo ndicho chanzo cha mtunzi wetu kusema;

mama yetu Afrika.
wanao tuateseka.
kwa majanga kutufika
wana wako Afrika.

Mtunzi wetu anamithilisha bara la Afrika na mama anaposema "Mama yetu Afrika" kwa kuwa mama huwa na huruma. Vilevile, ndiye atunzae wana wasipatwe na majanga hivyo basi anasihi Afrika ivikomeshe vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa ambavyo vita hivi vimesababisha waafrika kuteseka. Anasema "Wanao tuateseka" kuteseka huku kwa maana pana ni maangamizi, maafa, kupoteza makao na kuwa wakimbizi kutokana na vita na "Majanga kutufika" tashihisi hii ina maana kuwa waafrika wana shida nyingi zinazowakumba ambazo ni hatari kwa maisha yao. Kama vile tulivyoeleza hapo juu, vita vinavyohusisha bunduki vinasababisha maafa. Kwa kushadidia majanga haya King'ei anasema "Maisha yetu yatutoka". Usemi wenye maana kwamba wanapoteza uhai wao baadhi ya sababu ya vita hivi ni"tamaa kujitwika" hii ni ishara kwamba waafrika wana tamaa ya vitu mbalimbali vinavyosababisha vita hivi.

King'ei anaendelea kutumia taswira ya maovu yanayolikumba bara hili la Afrika, licha ya waafrika kuteseka kutokana na majanga mbalimbali na vita. Mtunzi anasema, "Mkoloni atucheka". Hii ni kinaya kwa ambavyo badala ya mkoloni kulisaidia bara la Afrika kujikwamua toka kwa majanga haya analicheka. Kando na majanga haya, mtunzi anaonyesha jinsi ukiukaji wa maadili ulivyosheheni katika bara hili.Anashadidia uovu kwa kusema "Ufisadi umewaka,"semi hii ina maana kuwa ufisadi umeenea sana barani Afrika. Kulingana na mtafiti, uozo huu ndicho chanzo cha mtunzi kusema;

> wana wako Afrika.
> utu wetu watutoka.
> uadui watukuka.
> kati yetu waafrika.

King'ei kwa kusema "Utu wetu watutoka" anashadidia uovu ulioshamiri barani Afrika. Kwamba, waafrika wamekosa utu na kukiuka maadili yanayohitajika katika jamii na

hivyo “Uadui watukuka” kunakosababisha kuchukiana na kutendeana maovu.Vile vile, kwa kusema kuwa “Uadui watukuka” ni kejeli kwa ambavyo waafrika wameenzi maovu kuliko kuenzi matendo yenye uadilifu. Kwa kushadidia utukufu huu wa uadui, anasema kwamba “Chuki yetu inawaka” semi hii inaashiria kuwa waafrika hawapendani na hivyo wana roho mbaya dhidi ya wenzao. Ndugu na ndugu wanadhulumiana vilevile baadhi ya watu wanawanyang’anya wengine vitu vyao kwa nguvu anaendelea kusema, “Visasi vingi kuweka” kwa maana ya kuwa na nia kulipa mabaya kwa yale waliyofanyiwa. Maovu haya kulingana na nukuu hii ni mengi kwa hivyo kudhihirisha uozo mwingi katika bara la Afrika. Kwa kushadidia uozo huu katika bara la Afrika King’ei anasema;

bara letu langulika
ndani yake linalika.
ni maradhi kulishika.
kwambukiza Afrika.

Tunamwona King’ei akiwa na umbuji mwingi katika ubeti huu anapowasilisha maudhui yake yenye uozo. Anasema kuwa “Bara letu langulika” kwa maana kuwa maovu yameenea barani na kusababisha bara hili lisiwe pahala pema pa kuishi hivi kwamba anaona kuwa “Ndani yake linalika” kwa maana kuwa maovu haya yanawaangamiza waafrika waishimo humo. Maovu haya yamesambazwa kote barani ndiyo maana anasema “Kwambukiza Afrika”.

Aidha, mtunzi anasema kuwa kuna majanga kama ufukara barani Afrika ambayo “Kote kote unawaka” kwa maana ya umaskini wa kutokuwa na pato la kutosha umeenea katika kila pembe barani Afrika. Kwa kutumia uradidi wa neno “kote kote” anasistiza jinsi ufukara huu ulivyoathiri bara la Afrika na kusababisha mateso kwa waafrika.

Vilevile, King'ei anasema kwamba baadhi ya maafa yanatokana na siasa ambazo hazijali utu zinazowanyang'anya waafrika uhuru wao. Rai hizi zinajitokeza katika ubeti ufuatao;

mauaji Afrika.
kila pembe yatapaka.
siasa zetu tupoka
huru wetu Afrika.

King'ei anatumia semi "Kila pembe yatapaka" kwa maana kuwa vifo vingi barani Afrika vimesababishwa na siasa potovu zisizojali utu na hivyo kuwanyima waafrika uhuru wao wa kujimudu na kuhusiana kama wana wa "Mama Afrika". Aidha, neno Afrika limerudiwarudiwa katika kila ubeti aghalabu mara moja, mbili hata mara tatu kwa nia ya kusizitiza na kuomboleza kwa ajili ya maovu yanayolikumba bara hili. Vilevile, anwani ya shairi hili "Afrika yaugua" ni jazanda kwa ambavyo kuugua ni kupatwa na ugonjwa. Yeyote anayeugua huwa na maumivu na hivyo huteseka, ni tanzia iwapo auguaye asipopata matibabu anaweza kuaga. Kwa hivyo, King'ei anaangazia maovu yanayolikumba bara la Afrika kuwa ndio ugonjwa unaosababisha mateso na mahangaiko kwa wanajamii. Aidha, anwani hii ya kijazanda ndiyo inayobeba ujumbe wa shairi nzima. Khatib katika shairi "Afrika" uk.6 lililo katika diwani ya *Wasakatonge.* Khatib anayaangazia matatizo ya kijamii yanayolikumba bara la Afrika. Khatib anaonyesha kuwa, maovu haya yameliandama bara hili la Afrika kwa muda mrefu na kwa hivyo anaona kuna umuhimu wa kuweka harakati za kuondoa uovu huo, japo anoana harakati hizi kuwa ngumu na zinahitaji tahadhari kubwa pamoja na umadhubuti, pia anahimiza kuchunguza mahali ambapo udhaifu ulitokea.

Katika ubeti wa kwanza mshairi anajiuliza kwamba ni lini Afrika itakuwa "Bustani ya Amani" taswira hii inaashiria kwamba Afrika bado inakabiliwa na vita na maovu

mbalimbali. Kwa hivyo bara hili limekuwa na dhiki si haba. Analiona bara hili kuwa kinyume cha matarajio yake kwa ambavyo badala ya kuwa bustani ya amani analiona kuwa Bustani ya ghasia, fujo na vita hivyo basi anaona si salama. Ndipo anasema "Ukabila kuuzika" semi hii inaashiria kuwa bara hili la Afrika limeshamiri watu wenye ukabila kwa hivyo anaona njia bora ni kuumaliza na kusahau ukabila huu kabisa. Vilevile, anaendelea kuangazia kuwa bara hili limeenea udini ambapo watu wenye imani inayohusiana na mambo ya kiroho baina ya binadamu na Mwenyezi Mungu wamejitenga kulinganana imani yao. Huu ndio uozo unaoendelezwa kupitia ukabila na udini.

Kulingana na mtunzi huyu udini huu umekita mizizi na umeenea kwa muda mrefu ndipo anauliza ni lini bara hili litamaliza maenezi ya udini huu?. Kwa umbuji wake, anatumia semi "Udini kuufyeka". Kwa maana ya kukomesha utengano unaotokana na imani mbalimbali kuhusu mambo ya kiroho. Vilevile, ni Jazanda inayoonyesha bara lililokumbwa na hali mbovu ya kijamii. Hivyo basi sanaa ina uwezo wa kusimulia mambo yanayohusiana na madili kwa mujibu wa nadharia ya maadili.

Mwandishi anakariri katika ubeti wa pili kuwa, Afrika ni bara lililojaa uovu na uonevu. Kwa hivyo anajiuliza uovu na uonevu huu utakwisha lini. Ndipo anasema, "Kufisha uonevu''semi hii ni masikitiko ya mtunzi kwa ambavyo angependa uonevu huu ukome "Kufisha" na hivyo bara la Afrika liwe "Ziwa la utulivu" hii ni jazanda inayoonyesha kuwa bara hili limejaa ghasia na mahangaiko kwa wanajamii yanayotokana na uovu na uonevu miogoni mwao. Huu ndio uozo unaoathiri jamii ambao Khatib angependa ukome kwa jamii kujenga maadili yanayokubalika kwa mujibu wa nadharia ya maadili



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

inayoshikilia kwamba, fasihi inaeleweka vyema inapohusishwa na mazingira ya jamii. Rai hizi zinajitokeza katika ubeti ufuatao;

lini?
Afrika utakuwa
ziwa la utulivu.
kufisha uonevu
kumaliza uovu
ni lini?

Khatib anendelea kuangazia bara la Afrika kama ambalo limejaa watu wenye chuki ambao hawapendani wala kupenda nchi zao. Mtunzi anajiuliza kuwa, ni lini Afrika itakuwa "Takia la upendo?". Hii ni taswira inayoonyesha kuwa bara la Afrika limejaa chuki ambapo watu wanakosa kuwa na mapenzi kwa wenzao hivyo basi wana roho mbaya. Mtunzi anapendekeza kuwa ili bara hili liweze kuwa takia la upendo lazima waafrika waweze "Kujenga uzalendo". Usemi huu ni himizo kuwa waafrika waweze kupenda nchi zao na bara lao na kuwa tayari kulirekebisha kwa kila hali ili liwe pahali pazuri pa kuishi kwa upendo. Katika ubeti huu, Khatib ametuonyesha uozo uliolikumba bara la Afrika kisha ametubainishia jinsi ya kukabiliana na uozo huu. Kwa kuwa sanaa ina uwezo wa kusimulia mambo yanayohusiana na maadili kwa mujibu wa nadharia ya maadili. Hivyo basi, kutuwezesha kuona namna uozo hasa chuki umeendelezwa katika jamii.

Mwandishi amechoshwa na uovu wa kuuana anawahimiza waafrika "Kuacha kuchinjana" Khatib anatumia semi hii kuonyesha dhuluma wanazofanyiana waafrika kwa kutendeana unyama usiojali utu. Ukatili wa kutoa watu uhai unatokana na kutopatana. Vilevile, Khatib anaonyesha kuwa bara hili lina watu wengi wenye maneno yanayoleta

ugomvi, uadui, chuki, na uchongezi baina ya watu ndipo anajiuliza iwapo bara la Afrika litakuwa 'Tamati ya fikina" mshairi anasema;

lini?
Afrika utakuwa
tamati ya fitina
kuacha kuchinjana
kuanza kupatana
ni lini?

Mwandishi ametumia taswira kwa kuuliza swali la balagha wakati ambapo bara la Afrika litakuwa "Radi yenye chereko" hii ni ishara kuwa Afrika imejaa shari tupu kwa kuwa hakuna raha wala furaha. Aidha, anakariri kuwa, bara hili limekumbwa na majanga si haba, anatoa mifano ya umaskini, njaa, magonjwa, ukame na mafuriko. Kwa umbuji wa aina yake anajiuliza siku ambayo Afrika itakuwa "Bwawa la utajiri" hii ni ishara kuwa Afrika inakabiliwa na umaskini mwingi na "Kufuta ufakiri." Usemi huu una maana ya kukomesha umaskini uliosheheni barani Afrika. Kwa hivyo, anataraji hali iwe nzuri iwapo umaskini huu utakoma kuwaangaisha wanajamii na hivyo Afrika itakuwa "Kitalu chenye shibe" kwa ambavyo watu wataweza kula na kupata shibe hivyo basi, "Na njaa isikabe" semi hii ina maana hawataweza kuwa na njaa tena kwa sababu ya shibe.

Aidha, anasema kuwa bara la Afrika limekabiliwa na magonjwa mbalimbali ndiposa anajiuliza kama bara hili litakuwa "Sayari ya uzima" ili liweze "Kupata siha njema" kwa ambavyo bara hili limeweza kutambulika kwa magonjwa na hivyo kulipa picha mbaya. Kulingana na mtunzi jambo hili litawezekana tu iwapo bara la Afrika litaweza "Magonjwa kuyazima" hii ni semi yenye maana ya kuyamaliza magonjwa yanayolikumba bara la Afrika. Vilevile, anajiuliza iwapo bara hili litakuwa "Adui wa ukame" semi yenye maana ya watu kukosa maji na hata mimea shambani hivyo basi

hairuhusu kitu kuota kwa sababu ya ukavu uliosheheni barani kwa kutumia tashihisi anasema, 'Kwa vyovyote uhame" hivi kwamba ukame huu upate suluhisho la kudumu ili usiwe kikwazo tena barani Afrika. Anaendelea kusema "Na usikuandame" tashhisi hii inaonyesha mwisho wa ukame huo kutorejea tena.

Kando na majanga haya, mwandishi anakariri kuwa Afrika ni "Nongwa ya mafuriko", yanayosababisha mahangaiko kwa wanajamii. Aidha, anaendelea kusema kuwa kuna madhara mengi barani Afrika ambapo waafrika hawana uhuru wao na hivyo wanakumbwa na dhiki. Mtunzi angependa Afrika iwe "Bikira wa uhuru" kwa kutumia swali la balagha anauliza wakati ambapo bara la Afrika litakuwa "Pepo ya dunia" kwa maana mahala pazuri ambapo "Raha kuogoleya" pana raha na furaha tele hivyo basi "dhiki kuzikimbiya" semi yenye matatizo na maovu kuisha.

Aidha, kwa umbuji wake Khatib anatumia maneno 'Lini?, Afrika utakuwana ni lini?' Katika mshororo wa kwanza, wa pili na wa sita mtawalia katika kila ubeti.Tunaona kuwa uradidi wa maneno haya ni msisitizo juu ya maovu yanayolikumba bara la Afrika. Aidha, katika neno la kwanza na la mwisho katika kila ubeti ni maswali ya balagha yaliyotumiwa kama kejeli kwa bara la Afrika kwa nia ya kuzindua msomaji atafakari pamoja na mtunzi ili aweze kuyaangalia maovu haya pamoja na mtunzi kwa ambavyo nadharia ya maadili inashikilia kuwa fasihi inaeleweka vyema inapohusishwa na mazingira ya kijamii. Hivyo basi, kutuwezesha kuona namna uozo huo unaathiri jamii.

Katika shairi "Uvundo" uk 77 lililo katika diwani ya *Miale ya Uzalendo.* King'ei anamulika jinsi jamii imeandamwana rushwa katika kila pembe ya maisha. Analipa shairi

hili anwani uvundo kijazanda kwa maana ya rushwa iliosakini katika jamii. Aidha, anwani hiyo ndiyo inaongoza ujumbe katika shairi nzima.

Katika ubeti wa kwanza mwandishi anakariri kuwa ufisadi umezagaa mijini na hata vijijini.Vilevile, anaendelea kusema kuwa pia kwenye zahanati ama hospitalini, unapokuwa u mgonjwa, "Hupati afueni." Semi hii ina maana kuwa hutibiwi ili uweze kupona kisa na maana "Mkono mtupu…". Hiki ni kipande cha methali yenye maana kuwa mwenye kutaka msaada pia hana budi kuwa tayari kuchangia.

Katika ubeti wa pili, anasema kuwa hata ukienda ofisini na hata mahakamani kwa kumshitaki mtu ama uwe ndiwe mlalamishi, uamuzi wa hakimu utakuwa wenye upendeleo kisa na maana "Dua la mnyonge…." hiki ni kipande cha methali yenye maana kuwa malalamiko yake mnyonge hayamtishi mwenye nguvu.

Mtunzi katika ubeti wa tatu vilevile anakariri kuwa unapokuwa hukumuni ukiwa unataka "Kujitoa hatiani" huwezi kamwe kujitoa kwenye hatia hiyo iwapo "Usizunguke mbuyuni." Semi hii ina maana kuwa usipotoa hongo utabaki pale kizimbani kwa sababu "Mti hauendi…." Methali hii ina maana kuwa hapana jambo kufaulu bila njia mahususi ya kulitekeleza. Kwa hivyo hongo ni njia ya pekee ya kujitoa hatiani.

Aidha, anabainisha kuwa hata kwenye maofisi unapokuwa kwenye shidauwe watafuta huduma sharti uweze kuwafisidi makarani ndipo upate huduma hiyo kwa kuwa"Mtakaa cha mvunguni …" methali hii ina maana kuwa mwenye haja fulani hana budi kuishughulikia au kuitaabikia haja yake ili itimizike.

Mahojiano kazini vilevile ni ya kirushwa, unapoyabaini maswali yote kwa kuyajibu yote hivyo basi huwa umefaulu lakini hutaipata kazi hiyo kwa kuwa "Damu nzito…" methali hii ina maana kuwa jamaa wa kuzaliwa pamoja husaidiana kila mara hasa wakati wa kutafuta kazi. Aidha, anaendelea kusema kuwa hata uwapo barabarani kwa matembezi "Watakutia mbaroni" kwa maana ya watakushika kwa kukudhani una nia mbaya kwa kuwa "Kuku wa maskini..." methali hii ina maana kuwa malalamiko ya mnyonge hayamtishi mwenye nguvu.

Aidha, anaendelea kusema kuwa siku hizi mapenzi yametawaliwa na pesa hivi kwamba iwapo una mapenzi moyoni yanayokuzonga akilini ilhali "Hamna kibindoni" kwa maana ya iwapo huna pesa za kuyanunua mapenzi huwezi ukadhaminiwa kwa kuwa "Bunduki bila risasi….." kwa maana ya hapana jambo kufaulu bila kulishughulikia kwa kushadidia maovu haya anasema kuwa uozo umesambaa kote nchini kwa kutumia swali la balagha ambalo vilevile analitumia kama kejeli. Anasema "Maovu wayatamani, wena autambua nani?" kwa maana ya kuwa watu wanadhamini sana uovu kuliko wema ambao ni kinyume cha maadili kwa mujibu wa nadharia ya maadili inayosema kwamba msanii huwa na dhamira ya kuandika yale yanayojenga jamii kimaadili kwa hivyo kubainisha majukumu ya mtunzi wetu katika kuirekebisha jamii. Rai hii inajitokeza katika ubeti ufuatao;

> nenda kote nchini, tembea bara na pwani
> maovu wayatamani, wema autambua nani?
> ni kauli ya duniani, ametuonya manani
> fisadi haiwezekani, yavunda bila ubani.

Kwa kutumia jazanda, King'ei anasema kuwa ufisadi umeenea kote na hivyo "Yavunda bila ubani" kwa maana ufisadi unadhihirika waziwazi kotekote bila kufichwa. Aidha,

mtunzi huyu kwa kulipa shairi hili anwani Uvundo ni jazanda inayoonyesha maovu yaliyoenea katika kila sekta ya maisha ya wanajamii. Aidha, anwani hii ndiyo inayoongoza ujumbe katika shairi nzima. Vilevile, kila ubeti umeanza kwa neno "Nenda." Neno hili limetumiwa kwa minajili ya kuonyesha kuwa rushwa imeenea kote nchini namna alivyoeleza katika ubeti wa mwisho hapo juu "Nenda kote nchini, tembea bara na pwani"

Katika shairi "Wake wenza" uk101 lililo katika diwani ya *Miale ya Uzalendo,* anabainisha maovu wanayotendeana wanawake walioolewa kwa mume mmoja. Katika ubeti wa kwanza bibi 1 anamweleza bibi 2 kuwa "Waniona kama nyanya" Tashibihi hii imetumiwa kumithilisha bibi 1 kuwa umri wake ni mkubwa na hivyo hapendezi. Aidha, anazidi kusema kuwa "Unazidi kuninyonya" kwa maana kuwa bibi 2 anamnyanyasa kwa kumpokonya mali waliyopata na mumewe kabla ya kumwoa bibi 2. Kwa hivyo amemsababishia ufukara. Rai hizi zinajitokeza katika ubeti ufuatao;

Bibi 1 bibi mdogo nakuonya
waniona kama nyanya
unazidi kuninyonya
nyumba wanifilisia.

Aidha, King'ei anabainisha katika ubeti wa pili kuwa kuna chuki baina ya bibi hao. Hivi kwamba, kila siku Bibi1 humpiza Bibi2 kwa hivyo " Uadui kukuza" kwa maana ya kuendeleza uadui baina yao ndiyo sababu Bibi 2 ameuliza "Kwa nini wanifatia?." Kwa maana wake hawa wanafanyiana madhila kwa sababu ya uadui uliopo baina yao. Vilevile, anaendelea kusema kuwa Bibi 1 anamweleza Bibi 2 kuwa mienendo yake si nzuri. Vilevile "Kiburi umekithiri" kwa maana ya kujiona kuwa yeye ni bora kuliko Bibi 1 na hivyo ana majivuno. Aidha, anadai kuwa humfanyia maovu mengi kwa kuwa ana wivu uliokithiri.

Kando na haya, Bibi 2 amemwonya Bibi 1 kwa kumtendea mabaya. Kwa hivyo, kumlaumu kwa sababu yeye ni mnyenyekevu wala hana wivu. Vilevile, hatumii nguvu ndiyo sababu anakejeli "Vipi wanilaumia?"Hali kadhalika Bibi1 anamweleza Bibi 2 kuwa kila mara "Huishi kwenda pembeni"kwa maana ya kwenda mahali pa siri hasa vichorochoroni na rafiki zake na hivyo kumfitini kuwa yeye ni mchawi pamoja na mambo mengi maovu.

Aidha Bibi 2 anamlaumu Bibi 1 kuwa hatulii nyumbani kwamasengenyo tele. Anatoa mfano kuwa Bibi 1 anadai kuwa hana nguo na uvumi tele. Vilevile, Bibi 1 anasema kuwa kinachomuudhi sana "Ni kumpokonya bwana" kwa maana ya kumchukua mume wake kwa nguvu aliyemzalia watoto na "Kwako umemfungia" kwa maana ya kumzuia asiende kwa Bibi 1 na hivyo basi kumtenga na mumewe kwa kutumia madawa za kumzunguka. Anasistiza kauli hii kwa kusema "Na madawa kumlisha."

Mshairi anaendelea kusema kuwa Bibi 2 anamkanya kwa kutomtunza mumewe kwa kusema kuwa "Bwanako kamwangalia" kwa kutompa mapenzi na kumchekesha kwa kutumia semi "Mapenzi kumwonyesha" atakapompa mapenzi basi "Chini utamketisha" kwa maana ya mumewe atampenda na kukaa naye nyumbani.

Aidha Bibi1 anamwona Bibi 2 kama mwenye wivu kwa kusema kuwa "Wanionea kijicho" kwa kuwa hana aibu anatumia semi "Wewe mkavu wa macho" kushadidia kauli yake. Kwa kuwa "Nyumba kunibomolea" semi hii ina maana kuwa anamvunjia mapenzi yake na mumewe. Tunaelezwa.

Bibi 1 wanionea kijicho
wewe mkavu wa macho
sijui unitakacho
nyumba kunibomolea.

Aidha, Bibi 2 anamlaumu Bibi 1 kwa kukatiza raha zao, kwa kuwa bwana ni wao wote sawia kwa kuwa pia naye bwana "Ndiye aliyeningiza" kwa maana kuwa pia sawasawa na Bibi 1 ameolewa kwa mume yuyo huyo. Hata hivyo Bibi 1 amemlaumu Bibi 2 kwa madharau yake na hivyo kumwomba "Heshima kuniwekea". Kwa maana ya amthamini na kumwekea adabu kwa kuwa yeye ndiye aliyekuwa "Wa mwanzo kuingia" kwa maana ya aliyeolewa wa mwanzo.

Kwa kulipa shairi hili anwani mke mwenza King'ei amebainisha maovu wanayotendeana wake hawa kwa minajili ya kutaka kupendeka mbele ya mume aliyewaoa kila mmoja akimlaumu mwenzake kuwa ndiye chanzo cha mapenzi yake kusorota juu ya mumewe. Aidha, anwani hii ni taswira inayoongoza ujumbe wa shairi nzima.

Aidha, King'ei anahimiza kuwa kwa kujenga jamii iliyo imara inahitaji heshima na kumwogopa Mungu aliyeumba dunia. Vilevile, kuyapima uyasemayo jinsi inavyojitokeza katika beti mbili za mwisho kwa ambavyo fasihi inaeleweka vyema inapohusishwa na mazingira ya kijamii hivyo basi kuonyesha namna uozo unajitokeza katika mashairi ya Khatib na King'ei.

Katika shairi "mbona mwateta?"uk23 Lililo katika diwani ya *Miale ya Uzalendo,* King'ei anaonyesha athari ya jamii kutengana kwa kukariri katika kibwagizo kuwa "Utengano ni adui" kwa ambavyo jamii yenye utengano huzua maovu tele jinsi itakavyobainika. Aidha, kichwa cha shairi ni taswira inayobeba ujumbe wa shairi nzima.

Katika ubeti wa kwanza mshairi anatumia ukinzani kuwa watu wanateta "Kucha kutwa mitaani" hii ni taashira ya kutokea kwa kutopatana kila wakati. Aidha, anakariri kuwa

daima wanasumbuana "Na chuki kufanyiana" semi hii ina maana kuwa wana roho mbaya na hivyo hawapendani. Wanaendelea kutakiana mabaya. Vilevile, hutoleana matusi na kulaumiana kila wakati aidha "Fitina mwatiliana" kwa maana ya kusababisha uadui na chuki miongoni mwa wanajamii.

Anaendelea kusema kuwa, mke namume hugombana kwa kukosa pesa za kukidhi mahitaji kama vile chakula na karo ya watoto shuleni. Aidha,kwa kukosa kupatana kunasababisha kupigana na hivyo "Hasara kutiana"kwa maana ya kusababisha upungufu na kuharibikiwa kwa vitu mbalimbali.

Kwa kukosa kupatana "Hatutasongea nchini" kwa maana ya kutopiga hatua za kimaendeleo na hivyo kudumu katika dhiki na kuwa kama wanyama kwa kukosa utu. Aidha, anaendelea kusema kuwa kwa kukosa kupatana kunasababisha "maovu kuapizana" kwa maana ya kutendeana mambo maovu. Kwa kuangazia masengenyo King'ei anasema "Vijembe mwatiliana" hata hivyo wanazidi kuwa na kijicho baina yao kwa kutumia semi "wivu kuoneana" kwa hivyo anapendekeza kusaidiana badala ya kushindana namna inavyojitokeza ubeti ufuatao:

kwa nini mnakosana, maovu kuapizana
vijembe mwatiliana na wivu kuoneana
heri kusaidiana, badala ya kushindana
nawaomba mpatane, utengano ni adui.

Ili kujenga jamii yenye maadili, King'ei anapendekeza kuepuka maovu kama vile ufitini, matata, kujiingiza kwenye lawama, visirani na tamaa. Anaendelea kuwasihi wazee kwa wana kupatana na "Tuache kuoneana" semi hii ina maana ya tusichukiane. Aidha anasema kuwa "masinzi kupakana" kwa maana ya kutendeana mambo maovu. Anashauri kuwa tusichekane na kuvunjiana heshima. Anaendelea kusema kuwa jamii isiwe yenye

vitisho wala kugombana katika uneni na hata mawazoni hii ndiyo sababu ya kusema "Chuki tuiweke chini" tashhisi hii ina maana kuwa jamii isiwe na kinyongo. Vilevile, anasema "Wivu tuondoeni" kwa maana kuwa jamii isiwe na kijicho miongoni mwao. Kwa kuwa utengano una hasara tele wala hakuna faida yoyote. Kwa hivyo anawashauri wanajamii kukutana kwa kuwa haifai kutetana. Hivyo basi, King'ei anahimiza jamii kujenga maadili yanayohitajika kwa ambavyo msanii huwa na dhamira ya kuandika yale yanayojenga jamii kimaadili hivyo basi kutubainishia majukumu ya mtunzi wetu katika kuirekebisha jamii yake.

Katika shairi "Tohara"uk2 lililo katika diwani ya *Wasakatonge.*Khatib anaonyesha namna tohara kwa mwanamke ina madhara na hivyo isiyofaa kutegelezwa kwa wanajamii; tahadhari hii anaitoa mtunzi kwa umbuji wake wa pekee ambapo anagawanya mishororo yake katika vipande vitatu venye mpagilio wa mizani mitatu kwenye kipande cha kwanza, mizani mitano katika kipande cha pili na hatimaye mizani minne katika kipande cha tatu.

Vilevile, kiitikio ni kifupi kinachobadilika kwa neno "Zinduka!" na "Amka!" kinaibua hisia kwa wasomaji waweze kutafakari pamoja na mtunzi kuona athari ya tohara kwa wanawake na kujukua msimamo unaofaa. Hata hivyo, anwani ya shairi hili ndiyo inayobeba maudhui ya shairi nzima.

Katika ubeti wa kwanza, Khatib anasema kwamba tohara kwa mwanamke ni hatari kwa kuwa ina madhara tele kwa uke wake; kwa kuwa husababisha hasara pekee inayoshamiri. Anaendelea katika ubeti wa pili kuwa jamii iweze kuepuka ngariba kwa kuwa ni "Wajuaji" hii ni ishara kuwa ngariba huwa wana hila za kuangaamiza jamii ndiyo sababu

Khatib anasema kuwa wao hufika na viroba vyao "Wachinjaji" kwa maana ya kukeketa uke wa mwanamke. Aidha, anaendelea kusema wanapofanya hivi hawana tiba ya kutibu vidonda wanavyovisababisha kwa hivyo ni "wauaji" kwa sababu wanasababisha maafa kwa wanajamii. Ubeti huu unatuchorea taswira akilini kudhihaki ngariba na kuonyesha kwamba tohara kwa mwanamke ni maangamizi. Khatib anatueleza;

epuka, hao ngariba, wajuaji,
hufika, navyo viroba, wachinjaji,
kumbuka, hawana tiba, wauaji
amka!

Mwandishi anakariri katika ubeti wa tatu kwa kutuchorea taswira ya namna ngariba hutekeleza tohara kwa mwanamke katika mazingira machafu.Anasema kuwa hutumia kiwembe kilichochafuka na kibubu kwa hivyo "Viumbe" kwa maana ya wanawake huathirika kutoka na kutu kwa hivyo anawazindua wanawake wajihadhari na ngariba. Vilevile, mwandishi anasema kwamba husababisha maradhi ya vidonda na pepopunda.Aidha, mwanamke anapokuwa na hedhi vidonda hivyo huchangia uke wake kuvunda. Isitoshe iwapo wembe ni mmoja na wari ni wengi "Ujuwa, ukimwi huja" tashhisi hii ina maana kuwa wari hao huambukizana ugonjwa wa ukimwi kupitia wembe wanaochinjiwa kwa mujibu wa shairi.

Mwandishi ametumia taswira kuwa mwanamke akeketwapo huwa taabani anapojifungua kwa kuwa ni vigumu kujitanua. Atasumbuliwa na misuli kwa hivyo anahimiza wanajamii kuacha "Mila dhaifu" kwa maana ya matendo maovu na hivyo anahimiza "Shikeni, uadilifu". Semi yenye maana kufuata maadili yanayohitajika katika jamii kwa mujibu wa nadharia ya maadili inayosema kuwa fasihi inaeleweka vyema inapohusishwa na

mazingira ya kijamii. Hivyo basi kutuwezesha kuona namna uozo hasa tohara ya wanawake inavyoathiri jamii.

Katika shairi "unyama" uk 47 lililo katika diwani ya *Wasakatonge,* Khatib anabainisha maovu ya binadamu. Kwa kulipa shairi hili kichwa unyama ni jazanda inayoashiria matendo maovu yasiyo na utu ayafanyayo binadamu. Vilevile, anaonyesha maovu haya katika ngazi zote za maisha. Aidha, kichwa hiki ndicho kinachobeba ujumbe wa shairi nzima.

Katika ubeti wa kwanza, mshairi anaangazia uovu wa binadamu hivi kwamba ni mkosa anayotenda maovu yasiyokadirika, kufikirika wala kusadikika ndiyo sababu anasema "Ni mnyama wa wanyama" kwa maana kuwa maovu yake yamezidi maovu ya wanyama wote.

Anaendelea kumchora binadamu kuwa dikteta anayetawala nchi kiimla. Vilevile, anatumia mbinu mbalimbali zenye hila hivyo binadamu kulingana na Khatib ni mkandamizaji. Aidha, binadamu ana vyombo mbalimbali ameweza hata kujenga mahakama na kuajiri polisi "Chungu nzima" kwa maana ya polisi wengi wa kumlinda. Vilevile, ameajiri jeshi la kuadhibu "Wakaidi" akiwa na maana ya kuwadhulumu binadamu wenzake wanaoenda kinyume na matakwa yake.

Binadamu amebainika kuwa ni mlafi kwa kuwa yeye hula vyakula kutoka baharini. Vilevile hula nyama zote za porini pia na mazao kutoka shambani na hata ndege warukao. Aidha, anaendelea kuangaliwa kama mwangamizi kwa kuwa huunda silaha

ambazo ni hatari ili kuathiri na kuangamiza binadamu wenzake ndio maana anasema "Dunia kuangamia"

Khatib anambainisha binadamu kama asiye na soni kwa sababu kwake ni kawaida kutenda maovu kama vile kuwabaka wasichana na kuwanajisi. Aidha, anawalawiti wavulana hivyo basi binadamu kulingana na Khatib ni "Mufilisi wa maadili" kwa maana kuwa anaenda kinyume cha maadili na huu ndio uozo anaobainisha khatib kwa kuwa umuhimu wa uadilifu ni kutovunja kiapo au kumsaliti marafiki kwa mujibu wa nadharia ya maadili. Rai hizi zinajitokeza katika ubeti ufuatao;

binadamu hana aibu,
ni kawaida kubaka,
wasichana kunajisi,
wavulana kulawiti
mufilisi wa maadili.

Binadamu Vilevile, anaonyeshwa kama anayemiliki vitu mbalimbali vinavyomsaidia kutenda maovu. Khatib anasema kuwa anayafuga majini na hata kuyatumia mashetani .Vilevile anaongea mizimuni ili aweze kuwadhuru wengine. Aidha, anasema kwamba binadamu alalapo na kuamka hujaribu kufika kila mahali ili "Dunia kuitawala" kwa maana ya kuwa na amri juu matendo na kila sehemu ya maisha ya watu. Anaendelea kusema kuwa, hata mwezini binadamu kafika kwa hivyo binadamu hatosheki hata hivi sasa anatafuta sayari ili atimize malengo yake ya "Kuendeleza unyama" kwa maana ya kufanya maovu zaidi dhidi ya binadamu wengine.

### 2.3. Kiishilio

Kupitia mashairi ya uozo kijamii wake wenza, makarani, polisi, wauguzi, mahakimu, ngariba, mume na mke katika ndoa wamesawiriwa kama wanaoendeleza uozo. Jamii

ikiwa na matarajio ya kutagusana na kuingiliana vyema kwa mienendo yenye maadili kinyume chake wanatengana na kutendeana maovu.Wao wamesawiriwa kama wauaji, wafitini,wala rushwa,warogi na wenye chuki. Vilevile, tumeomnyeshwa jinsi uozo wa kijamii ulivyoshughulikiwa katika kazi ya watunzi hawa. Hivyo basi, kuhimiza wanajamii kujenga maadili kwa mujibu wa nadharia ya maadili inayosema, sanaa ina uwezo wa kusimulia mambo yanayohusiana na maadili. Katika sura ya tatu tumelenga kuchanganua mashairi ya uozo wa kisiasa.

SURA YA TATU

# UCHANGANUZI WA UOZO KISIASA

## 3.1 Utangulizi

Katika sura ya pili, tumechanganua mashairi ya uozo kijamii. Katika sura hii tumenuia kuchanganua mashairi ya uozo kisiasa. Tumeshughulikia mashairi ya uozo kisiasa kwa lengo la kubainisha madhara yake kwa wanajamii. Aidha, tumeonyesha namna uozo wakisiasa umeendelezwa katika jamii kwa mujibu wa mashairi ya King'ei na Khatib. Isitoshe, katika mashairi ya uozo kisiasa tulionyesha wanaohusika katika kuendeleza uozo huo na kudhihirisha majukumu ya wasanii hawa katika kuirekebisha jamii kimaadili kwa mujibu wa nadharia ya maadili isemayo kwamba, sanaa ina uwezo wa kusimulia mambo yanayohusiana na maadili. Vilevile, Msanii huwa na dhamira ya kuandika yale yanayojenga jamii kimaadili. Sura hii pia imeongozwa na nadharia ya kimtindo isemayo kwamba huwezi kutenganisha ujumbe wa mtunzi na namna alivyoushughulikia.

Siasa inajihusisha na mitafaruku ya kijumla na njia za kusuluhisha mizozo hiyo. Mizozo huzuka kwa ajili ya sababu ya upungufu wa rasilmali, ili watu waendelee kuishi. Watu hubadilisha rasilmali kwa vitu wanavyohitaji. Lakini matarajio ya watu huwa mengi kuliko rasilmali zinazopatikana au wakati mwingine matarajio ya kikundi fulani yanaweza kuwa pingamizi kwa kikundi kingine.

## 3.2 Uozo wa Kisiasa

Mashairi katika kitengo hiki yameshughulikia viongozi wanaonyanyasa wapinzani wao, wanafiki, ubinafsi,wenye chuki, wanaoendeleza ukoloni mamboleo,wasaliti na tamaa.

Kuhusu viongozi madikteta, Khatib katika shairi "madikteta" iliyo katika diwani ya *Wakatonge* uk 21 anasema,

> madikteta.
> katika
> dunia hii ya tatu
> na hasa Afrika yetu
> itele "mungu watu"
> Bokasa, Idi, Mobutu
> mizinga nayo mitutu
> haitoi risasi
> hutoa maraisi
> walio madikteta

Anawaona viongozi kuwa wakatili, wanaotumia udikteta kwa kuwatawala watu wao. Anaeleza kuwa anajidai anayo nguvu ambazo hazitaisha milele kwa kuwalinganisha na "mungu watu". Hii ni jazanda inayoeleza dhihaka ya viongozi wasiojali umma.Vilevile anawalinganisha na 'Mizinga na risasi'Hii ni jazanda inayoashiria uongozi mbaya unaowagandamiza watu. Isitoshe, ni kinaya kwa ambavyo tunatarajia viongozi kuwajali wananchi kwa kuwapa huduma wanayostahili. Kwa hivyo, kudhihirisha tabia ya uongozi wenye uozo.

Tunapolihakiki shairi hili, tunaona kwamba Khatib kwa kulipa shairi hili anwani 'Madikteta' alidhamiria kuonyesha uongozi unaosisitiza kuwa kiongozi ni mtu mkubwa, mstahiki na hana nafasi ya kukosolewa na kwa hivyo anastahili kuabudiwa na binadamu kwa ambavyo anayo mamlaka ya juu zaidi ndiposa anawaita miungu watu. Kiongozi huyu huakikisha kuwa anajibari na watu ili wasiweze kumzoea na kumdharau na kuvunja amri zake, maana mazoea huleta dharau. Kwa vyovyote vile, mtu ambaye hukumzoea akikupa amri utaitekeleza haraka haraka si kwa kuwa umekiri uongozi wake bali kuitafuta heri yako. Kwa ambavyo anatawala kwa mizinga, risasi na mitutu. Khatib



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

anakuwa shupavu kiasi cha kumkabili kiongozi kwa kumkosoa na kuonyesha uozo wa viongozi kwa kusimulia mambo yanayohusiana na maadili.

Katika shairi "Hatukubali" lililo katika diwani ya *Wasakatonge* uk30. Viongozi vilevile, wanaendelea kumulikwa kama wenye kujilimbikizia mali, huku wanyonge wanaowatawala wakizidi kuungulika katika lindi la umaskini. mshairi anasema;

> hatukubali tena,
> kugeuzwa kuwa wajakazi,
> kugeuzwa kuwa wapagazi,
> kugeuzwa kuwa ni washenzi,
> hatukubali katu,
> ndani ya nchi yetu,
> iliyo huru.

Mshororo 'Hatukubali tena' umeanza na umerudiwarudiwa katika kila ubeti. Vilevile, mshororo wa nne katika kila ubeti ni 'Hatukubali katu'. Uradidi huu unanuia kusisitiza kuchoshwa kwa wananchi na uongozi huu wa mabavu usiojali maslahi ya wananchi.

Hali hii ya watu kuwa watumwa huku viongozi wakiwaongoza kwa kuwanyanyasa ni ugandamizaji na huu ndio uozo wa viongozi. Kwa hivyo, Khatib alikuwa na dhamira ya kuandika yale yanayojenga jamii kimaadili. Hivyo basi kuirekebisha jamii yake. Kwa ambavyo umma umeangaziwa kama wajakazi, wabagazi na kugeuzwa kuwa washenzi katika nchi yao iliyo huru huku viongozi wamejitukuza kwa kuwa mabwana.Wengine wao uongozi wao ushafika mwisho, ingawa masikitiko makubwa ni kwamba wale wanaokuja baada yao huwa hawana tofauti kubwa na walioondolewa. Hii ndiyo sababu ya Khatib kusema "Kwetu kurejesha"

Khatib anaendeleza vita vya ukombozi wa wanyonge kutoka kucha za viongozi mabarakala. Shairi hili ni mfano wa utunzi uonyeshao kutoridhika na utawala kaidi

wenye kutumia nguvu kunyanyasa raia. Mwandishi amebainisha utawala kama huo hauna nafasi sasa ndipo anasema 'Hatukubali tena'. Hali ya mtu mmoja kushiba kutokana na matunda ya shirika. Anabainisha ukoloni mamboleo na kunyanyaswa kwa wananchi. Vilevile, anaonyesha uongozi huu ameshindwa kujali utu. Kwa hivyo huu ndio uozo unaoenda kinyume na nadharia ya maadili inayoshikilia kuwa umuhimu wa uadilifu ni kutovunja kiapo au kusaliti marafiki kwa hivyo kubainisha viongozi kama wanaoendeleza uozo huo. Mtunzi huyu anaendelea kusema katika ubeti wa nne.

hatukubalitena
kutuletea usultani,
kutuletea na ukoloni,
kutuletea na uzayuni,
hatukubali katu,
ndani ya nchi yetu,
iliyo huru.

'Usultani, ukoloni, uzayuni' ni jazanda inayoonyesha usaliti wa uhuru uliopiganiwa na wananchi kwa kujitenga na kuwasahau wananchi hao Badala yake, kuendeleza mfumo wa kinyonyaji wa ukoloni mamboleo kwa kuzidi kuwanyonya na kuwakandamiza wananchi. Kwa hivyo raia wamechoka na kuchukizwa kwa kunyanyaswa. Khatib amehusisha utunzi wake na mazingira halisi ya jamii ambayo inadhulumiwa na viongozi wao kiasi kwamba wamekuwa vikwazo kwa raia hivyo basi kuonyesha namna uozo umeathiri jamii.

Khatib anaona dunia kama uwanja wa mapambano. Uwanja uliojaa "Mabwana" wachache na "Watwana'' wengi njia ya pekee ya kuleta usawa ni mapinduzi jinsi inavyojitokeza katika ubeti wa sita.

Khatib kwa umbuji wake anatumia semi 'Kula kiapo kulinda' kwa maana ya kuondoa unyanyasaji wa wanyonge. Jambo la muhimu sio kukata tamaa; wanyonge wanafaa

kukubali kuwa, licha ya maumivu kutoka kwa mabwana yafaa kuzidisha mapambano kwa kuwa ni juu ya wanyonge kujaribu kurekebisha hali zao na kujitanzua kutoka kwa uongozi usiojali utu. Dhima ya Khatib katika jamii yake ni, kuelekeza wanajamii palipo na dhuluma na kuweka wazi uovu huo ambao ni ngao madhubuti inayoweza kumlinda mnyonge dhidi ya kunyimwa na kuteswa na watawala wasiojali. Khatib anatumia jazanda ya 'Matunda' kwa maana ya kuleta usawa na kufaidi uhuru wao utakaopatikana tu kupitia mapinduzi yatakayoondoa utabaka na ukoloni mamboleo ulioenea.

Watunzi hawa wamewakabili viongozi wasio na utu.Tunapokuwa na hali hii yenye viongozi wengi wasiopenda kukosolewa, unafiki unatawala huku wananchi wanabaki wakiomboleza kwa ajili ya matendo ya watu wachache.

Kwa hivyo, watunzi hawa wanafahamisha umma uwe macho kwa kuangazia maovu ya viongozi wao ili waweze kuona tofauti iliyopo kati yao na watawala wao. Aidha, wanapendekeza hatua ambazo wanafaa kuzichukua baada ya kutafakari uovu huo ili uovu huo ukome na kujenga maadili kwa mujibu wa nadharia ya maadili isemayo kwamba, dhamira ya msanii ni kuandika yale yanayoijenga jamii kimaadili na hivyo kuonyesha namna uozo huo umeendelezwa katika jamii.

Khatib katika shairi "Nahodha," uk 41 lililo katika diwani ya *Wasakatonge*anasema,

> nahodha,
> wang'ang'ania sukani,
> michafuko, bahari siyo shuwari,
> si shuwari, pepo zinatuathiri,
> zaathiri, na mawimbi ni hatari,
> ni hatari, tufani meshamiri,
> meshamiri , na mvua zitiriri,
> zitiriri , radi nazo zikadiri,
> nahodha tosa nanga!

Katika shairi hili, tunamuona Khatib kwa akitoa tahadhari juu ya namna mambo yanavyoendeshwa. Anataka kuzindua nahodha wa chombo cha maji kama vile mashua, merikebu au meli. Huyu ndiye hutoa uamuzi wa mwisho wakati wowote ule ambapo chombo hicho huwa katika maji. Usalama wa mabaharia na wasafiri walio ndani ya chombo unategemea maamuzi ya mtu huyu.

Tunafahamu kwamba mara nyingi katika vyombo vikubwa wapo wasaidizi wa nahodha, ipo hatari kwamba hawatasikizana. Hali hii ya kutosikizana yaweza kuzua matatizo mengi katika meli na huenda pengine kukawa na vifo baada ya kuzama kwa meli hiyo, Khatib anatuambia kwamba 'Nahodha tosa nanga'. Kauli hii ndio kitovu cha ujumbe unaopatikana katika shairi hili.

Tunaweza kuona kwamba ujumbe huu unatuwasilishia uozo uliopo katika baadhi ya taasisi zetu, katika maafisi, biashara na utawala wa nchi huwa tunafahamu kuwa lazima kuwe na viongozi kwa hivyo neno 'nahodha' limetumika kijazanda kuashiria viongozi. Mathalani katika nchi lazima kuwe na waziri mkuu, rais au mfalme. Ni huyu mkuu wa nchi ambaye ana jukumu la kuhakikisha kwamba mambo yote yanakwenda kama yanavyotakikana.

Ujumbe wa shairi unaweza kuchukuliwa kwamba umfikie mtu wa aina hii. Mwandishi anajaribu kuonyesha kuwa mambo ya serikali kwa mfano hayawezi kushughulikiwa na yatengenee ipasavyo na watu wengi wakati ambapo mkuu wa nchi hawajibiki ipasavyo.

Baada ya ujumbe huu kueleweka inabidi tutafakari zaidi ya umbuji wa Khatib katika shairi hili. Ni muhimu tuone kwamba kwa kuendeleza mitindo yake mipya ya mipangilio ya mizani, tuanaona jinsi alivyogawanya mistari. Inatubidi tutaje kwamba kila mstari wa

ubeti huo unajitosheleza. Unaposoma kila mshororo unaona kwamba una ujumbe maalum. Aidha neno la mwisho katika mshororo ndilo linaloanza mshororo unaofuata. Maana nzima ya shairi inajitokeza baada ya kusoma mstari wa mwisho.

Tunaona kuwa Khatib anatetea haki za wanyonge ambao wanadhulumiwa na viongozi wao. Pia anaonyesha taabu za wananchi kwa kutumia neno 'Michafuko'kijazanda vilevile, amebaini uongozi ambao una changamoto nyingi kwa mfano anasema,'bahari si shwari,pepo zinatuathiri, tufani, mvua, radi' maneno haya yametumika kijazanda kuashiria maongozi yasiyofaa ambapo viongozi wanasozania uongozi na hivyo kusababisha kuzembea katika nyadhfa zao na kutowajibika kwa kutenda haki. Huu ndio uozo katika uongozi ambapo mamlaka yamewabadili viongozi wakawa tofauti kihulka na maadili. Khatib amesimulia mambo haya yanayohusiana na maadili ili kutuonyesha namna uozo wa viongozi umeendelezwa katika jamii ambayo kinadharia wana uhuru lakini kimatendo wamo kifungoni.Kwa hivyo kuwamuru viongozi kujirekebisha na kujenga maadili kwa ambavyo umuhimu wa uadilifu ni kutovunja kiapo au kusaliti marafiki.

Tunatambua kuwa kazi ya Khatib inadhihirisha ulimwengu anaoandikia umetawaliwa na uongozi wenye shari tupu. Japo wananchi wana tamaa ya heri ambayo ndiyo pekee inaweza kusaidia kuwawezesha waafrika na wanyonge wote wa ulimwengu wa tatu kupata ufanisi bora katika juhudi zao za kuendeleza maisha yao. Hivyo basi, kuirekebisha jamii yake kimaadili kwa ambavyo dhamira ya msanii ni kuandika yale yanayojenga jamii kimaadili.

Aidha, katika shairi hili mtunzi anatujengea taswira ya nahodha, abiria wakiwa ndani ya chombo cha majini, abiria tunawaona wakiteseka. Tumechorewa picha ya abiria ambao wamelewa huku wanatapika. Kati ya abiria hawa ni akina mama, wakongwe na hata watoto. Kwa hivyo jamii nzima inateseka ilhali nahodha hawajali.

Kupitia shairi hili, Khatib amewasawiri viongozi kama wasaliti na wasiojali maslahi ya wananchi.wanang'ang'ania mamlaka licha ya wananchi kutoridhishwa na uongozi wao. Hawataki kung'atuka kutoka kwenye nyadhifa walizoshikilia. Kwa hivyo,Khatib anawakejeli viongozi waliochaguliwa kuleta maendeleo badala yake wamesababisha mahangaiko kwa wanajamii hasa wakongwe, akina mama na watoto. Wanajamii wameshuhudia ulafi wa viongozi wa kutaka kujinufaisha. Hivyo basi, Khatib anawahimiza viongozi kujenga maadili kwa kuwajibikia jamii. Kwa hivyo, ametuonyesha namna uozo unaathiri jamii kwa ambavyo fasihi inaeleweka vyema inapohusishwa na mazingira ya jamii kwa mujibu wa nadharia ya maadili.

Katika shairi "Ndumakuwili" uk 155 lililo katika diwani ya *Miale ya Uzalendo*, king'ei anaangazia ulafi na unafiki wa wanasiasa anasema;

> ndumakuwili mfano, kiongozi ofisini
> kujitakia vinono, wenzake kutothamini
> huyakenua meno, "mzalendo namba wani"
> hakika ndumakuwili, ni adui wa jamii

King'ei ametumia jazanda 'Ndumakuwili'kwa kawaida ndumakuwili ni kiumbe afananaye na nyoka husemwa ana vichwa viwili. Katika muktadha huu ndumakuwili ni mtu ajifanyaye mwema kumbe sivyo. Mtu ajifanyaye rafiki kumbe ni msaliti. King'ei ametumia neno hili ili kuwasawiri viongozi ambao ni wanafiki na vigeugeu. Anasema 'Kujitakia vinono'ni semi yenye maana ya tamaa zao kutaka kujinufainisha. Huku

'Wakiyakenua meno' vilevile, ni semi yenye maaana ya kuwahadaa wananchi kuwa wao ndio wazalendo wakuu wanaopenda nchi yao. Aidha, neno ndumakuwili limerudiwarudiwa katika kila ubeti, uradidi huu unanuia kusisitiza unafiki wa viongozi kwa kutokuwa wa kweli kwa ambavyo wanasababisha jamii kuumia. Vilevile, anasema kwamba "Hana mbele wala nyuma". Semi hii ina maana kuwa mtu mwenye mienendo kama hii hawezi akaaminika kwa ambavyo anayoyatenda lazima kuwe na shaka ambapo unafaa kuyapima kwanza. Huu ni uozo wa viongozi kwa ambavyo nadharia ya maadili inashikilia kwamba umuhimu wa maadili ni kutovunja kiapo au kusaliti marafiki.

Ni bayana kuwa viongozi hapa wanaangaliwa kama wasaliti na wanafiki wakubwa. King'ei anawasawiri viongozi kama wabinafsi, wenye chuki, wazembe na wenye kiburi. Ni kinaya kuwa viongozi waliochaguliwa kuleta maendeleo badala yake wanasababisha mahangaiko kwa wanajamii. King'ei ameshuhudia unafiki wa viongozi wa kutaka kujinufaisha. Mtunzi huyu amekosa amani kwao ndiposa hataki kuwahusisha na uzalendo na kuwaona kuwa adui wa jamii.

Katika shairi "Kinyume cha katiba" uk 82 katika diwani ya *Miale ya Uzalendo* King'ei anaonyesha namna wananchi wana majuto ya kupata viongozi wenye tabia za uozo kama viongozi wa hapo awali wenye kutawala badala ya kuongoza. pale ambapo wananchi wanatawaliwa hawaongozwi, wanalazimishwa kufuata sera fulani bila kupewa mwelekeo unaofaa. Vilevile, wanabainika kuwa wanafiki wakubwa kwa vile wakoloni walipotoka tunawaona hawajali tena kuendelea na azma yao ya kuleta hali ya maendeleo bali wao wanang'ang'ania uongozi kwa nia ya kujifaidi. King'ei anasema;

katiba itupe tawala
tawala za mabavu
kutawala sio kuongoza
hatutaki kuongozwa
hatujapata viongozi
tumepata watawala
mkoloni tumemng'oa
twajitawala wenyewe

Anwani ya shairi hili'Kinyume cha katiba' ni kinaya kwa ambavyo ni kinyume cha matarajio. King'ei amechora taswira ya katiba ambayo haijali utu wala haki. yenye ukatili na ujangili, katiba ya wenye shibe isiyo na haki ila unafiki, isiyofuata sheria ila hongo, katiba ya ujinga, inayotetea tawala za mabavu, katiba ya uhuni. kwa hivyo katiba hii haiwapi wanaoongozwa tumaini lolote. Huu ni uozo wa katiba kwa ambavyo badala ya katiba kuwafaa wananchi wote inawafaa wachache ambacho ni kinyume cha uadilifu. Anapendekeza katiba inayojali utu na haki,inayolinda na kushughulikia haki na maslahi ya raia, katiba inayofuata sheria, katiba ya kuondoa ujinga anaendelea kupendekeza katiba ya kuondoa utawala wa kimabavu, unafiki na ufisadi, katiba isiyo ya wachache wateule, katiba ya kuondoa utabaka na ukaloni mamboleo.

King'ei anasema 'Hili dude 'katiba'neno dude kwa kawaida hutumiwa kuita kitu kikubwa ambacho mtu hana uhakika wa jina lake mahsusi. Aidha, hutumiwa kuitia kitu au mtu unayemdharau na usiyetaka kumwita kwa jina lake la kawaida. Katika muktadha huu, King'ei anakejeli katiba kwa ambavyo haijali utu wala haki. Vilevile, anasema 'Katiba ya kuzunguka mbuyu'Semi hii ina maana ya kuhonga au kutoa rushwa. Kwa hivyo kudhihirisha uozo. Kwa kushadidia uozo huu, anatumia swali la balagha 'Hii ndiyo katiba?'Hii ni dhihaka kwa ambavyo badala ya katiba kujali utu na haki kwa

kushughulikia maslahi ya raia, katiba hii haiwajali raia ila inaendeleza tawala za mabavu hivyo kuwa na ukatili kwa raia huku ikiwalinda wateule.

King'ei anatumia jazanda 'Tawala za mabavu' kuashiria uongozi unaotumia nguvu sizizo na kikomo. Wanatumia nyadhifa kukidhi haja zao licha ya kumwondoa mkoloni bado utawala unaendelezwa na viongozi wa Afrika

Walipoondoka wakoloni, wananchi walitarajia kuwa wangepata viongozi kuyajali maslahi yao. Hawakujua kuwa wangebadilisha tabia zao na kufuata utawala wa wakoloni. Raia wa nchi wa ulimwengu wa tatu walikuwa na matumaini ya maendeleo ya uhuru. Hata hivyo mara nyingi matumaini yao yamegeuzwa ndoto ya jinamizi. Viongozi na watendaji wengine wanaendeleza raha zao kwa kutumia jasho la raia. Shairi hili linapiga vita ukoloni mamboleo katika mataifa huru ya kiafrika.

Katika shairi "Miamba" uk 29 katika diwani ya *Wasakatonge.*Khatib anatumia jazanda ya wanyama kuonyesha uhalisia wa uozo wa binadamu hasa wenye mamlaka kwa wanyonge anasema;

miamba
chui na simba
mbugani wanatamba
vinyama vinayumba
chakula cha wakubwa
ni sheria za mbuga?

Anwani ya shari hili 'Miamba' ni jazanda kwa ambavyo mwamba ni mtambao wa jiwe au jabali lililoko baharini chini ya maji. Kwa muktadha huu, miamba ni viongozi wanaojitukuza na kujitenga na umma na kuwatawala kiimla.

Mtunzi huyu anatumia semi anawataja wanyama kama chui na simba kuwa 'Mbugani wanatamba'huku vinyama vidogo vikihangaika. Kwa maana wanaenda huku na huko kwa kujigamba. Hii ni ishara ya kutawala kwa mabavu huku watawaliwa wakiishi kwa hofu kwa kushurutishwa.

Tunapolihakiki shairi hili, tunaona kuwa walio na mamlaka ya juu ndio wanaonasibishwa na chui na simba. Wanawadhulumu wanyonge ambao wamenasibishwa na digidigi na nyani. Khatib ametumia wanyama kuangazia jinsi wenye mamlaka na uwezo wanavyowadhulumu na kuwagandamiza wasio na uwezo. "Ni sheria za mbuga?" swali hili ni kejeli kwa viongozi ambao wanapaswa kuwa vielelezo vyema kubadili majukumu yao na kuanza kujali maslahi yao binafsi huku wakiwakandamiza wanyonge.

Aidha, Khatib katika shairi 'Wafadhiliwa'uk38 lililo katika diwani ya *Wasakatonge.* anaendelea kuwakashifu viongozi kama wasaliti, wenye tamaa ya mali na wanafiki. Kwa hivyo kuvunja nemsi ya uaminifu kwa wananchi. Huku wakibadilisha vifungu vya katiba ili kujinufaisha. Mshairi anasema,

> Wafadhili kufurahishwa
> ni sera zao kupitishwa
> rais anaamrishwa
> tekeleza!
> mawaziri wanajulishwa
>
> Sheria zinabadilishwa
> na bungeni kuhalalishwa
> pitisheni!

Anwani ya shairi hili 'Wafadhiliwa' ni kinaya kwa ambavyo viongozi hawa wamesaidiwa kwa ukarimu wa wananchi lakini tunawaona haja yao ni kutaka kujinufaisha kibinafsi ila sio kuhudumia umma. Vilevile, anatumia nidaa 'Tekeleza! Pitisheni!'ni hisia anayotumia mtunzi kama kejeli kuonyesha kwamba hakuna

demokrasia bali maangamizi, dhuluma na utawala wa kiimla wa viongozi kama vile Rais,Wabunge na Mawaziri. Aidha, mtunzi anaendelea kusema kuwa 'Uhuru wetu twauuza' ni semi yenye maana kuwa na viongozi ambao hawajali maslahi ya umma ambao vilevile viongozi wasio na utu. Kwa hivyo anawakebehi viongozi wa wakati huo.

Katika shairi hili, Khatib anawabainisha wanasiasa kama wanafiki, waongo na wenye tamaa. Wanabadilisha vifungu vya sheria na kumwamrisha rais kutekeleza, sheria ambazo zimetungwa kuwadhulumu wananchi bila hata wao kushirikishwa. Kwa hivyo, ni sheria zinazotetea maslahi ya watu wachache huku umma ukigandamizwa.

Katika shairi 'Wafrika unganeni'uk13.lililo katika diwani ya *Miale ya Uzalendo.* Kinge'i anaona kuwa Maamuzi ya kutokubali kunaswa tena na janja na hali za wakoloni mamboleo siyo rahisi kuyafikia. Ni maamuzi yanayohitaji ujasiri mkubwa na moyo thabiti. Aidha King'ei anafahamu matatizo yanayolikabili na yatakayolikabili bara la Afrika siku za usoni kama litakubali kuuza uhuru wake sasa, mshairi anasema,

> Mkoloni 'liondoka
> ingawa hakutoweka
> bara letu Afrika
> ukoloni waonekana
> pembe nyingi angalia

Mtunzi ametumia jazanda 'Mkoloni 'liondoka ingawa hakutoweka'kukashifu ukoloni mamboleo ambapo hulka za viongozi si halisi. Wamesaliti uhuru uliopiganiwa na wananchi kwa kujitenga na kuwasahau wananchi hao. Badala yake wanashirikiana na mfumo wa kinyonyaji wa ukoloni mamboleo kuzidi kuwanyonya na kuwagandamiza wananchi wa tabaka la chini. Mtunzi anaonyesha kwamba viongozi walitarajiwa

kurekebisha na kuondoa athari za kikoloni kinaya ni kuwa wao ndio wanaosaidia kuendeleza athari hizo.

Vilevile, mtunzi anatumia semi 'Watunyonya yetu damu'kunyonya kwa kawaida ni kuvuta kitu kiowevu kwa mdomo.Katika muktadha huu, kunyonya damu ni kutegemea wafrika kwa kuwanyanyasa huku wakiwadhulumu katika ngazi zote za maisha huku wakiwaacha maskini. King'ei kwa kushadidia athari za ukoloni anatoa mifano ya Afrika kusini ambapo anatuchorea taswira ya weusi wanaotaabika kwa kubaguliwa katika ngazi zote iwe nyumbani au kazini wanadunishwa na makaburu.Vilevile, anasema kuwa maisha yao yamo hatarini kwa ambavyo wamedunishwa waziwazi, kuuliwa ovyoovyo na kuwatumikia weupe kwa hivyo wana huzuni. Kando na Afrika kusini, mtunzi huyu anatuchorea taswira ya nchi ya Namibia ambayo ukoloni mamboleo umekita mizizi na kuwafanya waafrika kuwa watumwa.

Shairi hili linapiga vita ukoloni mamboleo katika mataifa huru ya kiafrika. Mtunzi amedhihirisha kwamba, sera hiyo ni hatari kwa ustawi wa nchi yoyote ile. Kwa hivyo suluhisho ni kukomesha mfumo huo uliojaa dhuluma, unyonyaji, maonevu, kudharauliwa, kukandamizwa kwa waafrika kwa kuungana. Kwa hivyo, viongozi wa Afrika wanahimiswa kujenga maadili kwa mujibu wa nadharia ya maadili inayoshikilia kwamba, fasihi inaeleweka vyema inapohusishwa na mazingira ya jamii. Hivyo basi, kuonyesha namna uozo wa ukoloni mamboleo unaathiri jamii.

King'ei katika shairi 'Uzuzu'uk120. lililo katika diwani ya *Wasakatonge*. Anaendelea kuwa wakili wa wanyonge wengi ambao daima wamebaki wakinyanyaswa na wenye nguvu. King'ei anasema;

> Walopata uongozi, baadhi walilegea
> ikiwa mali kuozi, tamaa kuwakolea
> wakaidharau kazi, kwa pato kulizegea
> uwezo na utukufu, visituzuzue jama

King'ei anafumba ujumbe wake kwa kutumia semi 'Mali kuozi, tamaa kukolea' kwa maana ya kuwa na hamu kuu ya kujilimbikizia mali. Mtunzi anatumia semi anaposema "Wongozi tuliposhika" kwa kawaida shika ni kukamata kitu. Kwa hivyo, katika muktadha huu wongozi kushika ni semi iliyotumiwa kuonyesha kupata mamlaka ya kuelekeza umma. Anaendelea kusema kwamba viongozi waafrika walioshika hatamu baada ya wakoloni kwenda waliwabagua waafrika wenzao kwa kudhamini vyeo vyao huku wakikosa kuujali umma kabisa kwa kujitenga nao bila kuwafaa kwa lolote.

Aidha, viongozi wamemulikwa kuwa tajiri huku umma ukiwa maskini.Walio kwenye mamlaka wakaingiwa na tamaa pamoja na chuki kwa ambavyo hawakutaka wanaoongozwa pia kuongoza ili wasiweze kupanda ngazi ya utabaka. Hii ndio sababu anatumia tashbihi "Kuwaka ja pilipili" Hii inadhihihirisha kwamba viongozi huwa wakali kukabiliana na yeyote anayetaka kukabili vyeo kwa kuwa wana chuki na tamaa ya uongozi.

King'ei anaendelea kusema "Waloketi kwenye viti" Hii ni semi yenye maana ya walio kwenye uongozi ambao wanawadhulumu wanaoongozwa licha ya uongozi wao kuwa mbaya hawataki kuwabisha wengine, wanaendelea kuwagandamiza wasio na vyeo ili

wasivipate. Kwa hivyo, wamekuwa vikwazo au vizuizi vya wengi walio chini ya utawala wao.

Huu ni mfano wa viongozi waliojitenga na umma ili kushirikiana wenyewe kuzidi kuwanyonya na kuwagandamiza wananchi wa tabaka la chini.Viongozi kama hawa wanasaliti uhuru wa nchi zao. Hawajali maslahi ya umma bali yao binafsi yanayowafanya kuwagandamiza wananchi. Viongozi kama hawa tunavyochorewa katika shairi hili hawana mawasiliano mema na jamii wanazohudumia. King'ei anaangazia kuzuka kwa dhuluma, unyanyasaji na unyonyaji wa umma ni kutokana na viongozi kung'ang'ania uongozi na kujilimbikizia mali. Tunaona mtunzi akikariri katika kibwagizo "Uwezo na utukufu,visituzuzue jama". Uradidi huu unaashiria kwamba viongozi walitumia vibaya mamlaka yao. Waligeuka wanyama na kuwadhulumu wananchi baada ya kutwaa hatamu kutoka kwa wakoloni. Mienendo ya viongozi ni mibaya mno,haja yao ni kujinufaisha kibinafsi na sio kuhudumia umma. Kwa ambavyo dhamira ya mtunzi wetu ni kuandika yale yanayojenga jamii kimaadili ili kuweza kuirekebisha jamii yake kutoka kwenye mienendo yenye uozo kwa mujibu wa nadharia ya maadili.

Watunzi hawa wanavunja kimya kwa kuonyesha jinsi jamii inavyonyanyaswa na viongozi wasiowajali. Wanauona ukimya kama jambo la hatari kabisa. Kwa hivyo, wanatumia, ushairi kama fimbo ya kufichua uovu wa viongozi hao. Wanafahamu kuwa kwa kuogopa kunena juu ya uvundo huu hali waliondani itaendelea kudumu. Aidha, wanafahamu kutonena kutawanufaisha viongozi wanyonyaji. Vilevile, mtu mmoja

anapojitokeza na kunena waziwazi, huwa amesaidia sana katika kuirekebisha hali ya watu wengi.

### 3.3 Kiishilio

Kupitia mashairi ya uozo kisiasa, wabunge, mawaziri, rais na viongozi katika taasisi mbalimbali ni viongozi mamlakani ambao wamesawiriwa kama wamepotoka kimaadili. Jamii ikiwa na matarajio kuwa wangeongozwa kwa mienendo yenye maadili kinyume chake viongozi hawa hawajawajibika. Wao wamesawiriwa kama wabinafsi, wasaliti, wenye tamaa, wabaguzi, wenye chuki na wanafiki.Vilevile, tumeonyesha namna watunzi wetu walivyosawiri uozo katika kazi zao na hivyo kubainisha jukumu lao katika kuirekebisha jamii kimaadili kwa mujibu wa nadharia ya maadili. Katika sura ya nne tumelenga kuchanganua mashairi ya uozo kiuchumi.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## SURA YA NNE

## UCHUNGUZI WA UOZO KIUCHUMI

### 4.1 Utangulizi

Katika sura ya tatu tumechanganua mashairi ya uozo kisiasa. Katika sura hii, tumechanganua mashairi ya uozo kiuchumi kwa lengo la kuchanganua uozo katika mashairi ya Khatib na King'ei yalivyoathiri jamii kiuchumi. Aidha, tumebainisha namna uozo wa kiuchumi ulivyoendelezwa. Vilevile, kuonyesha wanaohusika katika kuendeleza uozo huo. Isitoshe, tumedhihirisha namna washairi wetu walivyosawiri uozo wa kiuchumi katika mashairi yao. Kisha, tumeonyesha jukumu la wasanii wetu katika kurekebisha jamii yenye uozo wa kiuchumi ili kujenga maadili kwa mujibu wa nadharia ya maadili isemayo kwamba msanii huwa na dhamira ya kuandika yale yanayojenga jamii kimaadili.

### 4.2 Uozo Kiuchumi

Mashairi katika kitengo hiki yameshughulikia wanajamii ambao wamepotoka kimaadili. Msingi wake ni kuwa, hawawezi kutambua uwezo wao wa kuzalisha mali huku wakiwa na tamaa ya kuwa na hali au maisha ya namna fulani. Hata kama itawabidi kuwadhulumu binadamu wenzao.

Katika shairi "Hatuna kauli" uk 8 lililo katika diwani *ya Wasakatonge* mshairi anabainisha unyonyaji wa uchumi wa Afrika. Anaonyesha mivutano baina ya bara Ulaya na bara Afrika ambapo bara Ulaya linabainika kuwa linanyonya jasho la Afrika. Vilevile, anatuonyesha kwamba waafrika wanafanya kazi za sulubu kama vile shambani na hata viwandani kwa manufaa ya bara la Ulaya. Unyonyaji huu unalifanya bara Ulaya kutajirika kwa jasho la Afrika. Taswira inayojitokeza ni ya unyonyaji na unyanyasaji.

Anaangazia unyonyaji huu katika pande zote katika bara la Afrika, anasema "Si umma si serikali". Kwa kutumia neno **'si'** Khatib anasisitiza kuenea kwa unyonyaji huu wa kiuchumi na hivyo kudhihirisha ukoloni mamboleo. Shairi hili kwa hivyo limedhihirisha waafrika walivyomatesoni, wanaofaidi matunda ya kazi ngumu ni wazungu na hivyo kunyonywa na kuteseka kwa waafrika.

Mshairi anasema kuwa, waafrika wanaletewa sera, kupangiwa mipango na hata kupewa maagizo pamoja na amri kutekeleza. Maneno haya yanadhihirisha ukoloni mamboleo wenye dhima ya kunyonya jasho la waafrika. Kwa kushadidia unyonyaji huu katika ubeti wa nne anatumia semi "Mipango tunapangiwa" kwa maana ya kuweka sera zao za unyonyaji kwa utaratibu jinsi inavyojitokeza,

> maagizo tumepewa,
> mipango tumepangiwa,
> na amri tunatolewa.

Tunamwona Khatib anaomboleza na waafrika kuwa, nguvu zao nyingi zimetumika bila kupata chochote ambacho kina faida kwa waafrika. Kwa hivyo, ameweza kutambua uonevu huu wa wazungu ambao unatumia ulaghai na mabavu. Mtunzi huyu anakosoa bara Ulaya linalowanyanyasa waafrika kujenga maadili kwa mujibu wa nadharia ya maadili inayoshikilia kuwa umuhimu wa uadilifu ni kutovunja kiapo au kusaliti marafiki. Hivyo basi kuonyesha bara Ulaya kama lililokiuka maadili ya kiuchumi.

Aidha, anasema kuwa "Sera zote siyo zetu" hii ni taswira ya uchumi wa kibepari na hivyo hakuna neema kwa mafukara waafrika, kwa ambavyo hawafaidi matunda ya uhuru wao. Mwandishi anaonyesha kuwa uhuru waliopata hufai chochote kwa kuwa unyonyaji unaendelea jinsi anavyobainisha;

zatumika nguvu zetu,
bila yakupata kitu,
chenye faida kwetu,

Vilevile, Khatib anadhihirisha kuwa hakuna usawa wa kiuchumi miongoni mwa bara la Ulaya na Afrika kwa ambavyo waafrika hawakuondolewa unyonyaji baada ya uhuru. Anaendelea kusema kwamba, vitu vinavyoagizwa kutoka bara la Ulaya huwa na bei za thamani kinyume na bidhaa zinazoagizwa Afrika kwenda Ulaya ambako bei huwa duni. Ubinafsi unaojitokeza katika shairi hili unaambatana na unyonyaji usiojali utu. Ulimbikizi huu wa mali unabainisha kunyonya waliozalisha mali pia utumizi wa hila ili kuwazugazuga wanyonge na kuamwa jasho lao hali hii ya ubinafsi inavunja hali ya kiutu.

Kwa jumla, Khatib kwa kulipa shairi kichwa "Hatuna kauli" ni jazanda inayoongoza ujumbe wa shairi nzima. Katika shairi hili Khatib anaonyesha matatizo yanayolikumba bara la Afrika kutokana na hali ngumu ya maisha. Anadhihirisha kwamba uchumi wa bara la Afrika umeathiriwa na sera za bara ulaya na hivyo kusababisha hekaheka nyingi kwa waafrika. Khatib kwa hivyo, anahimiza bara Ulaya kujenga maadili kwa mujibu wa nadharia ya maadili inayosema, fasihi inaeleweka vyema inapohusishwa na mazingira ya jamii. Hivyo basi, kuonyesha namna uozo wa kiuchumi umeathiri bara la Afrika.

Aidha katika shairi "Acheni milimbiko" uk 25 lililo katika *Miale ya Uzalendo,* King'ei amebainisha tamaa ya mali anasema kuwa baadhi ya watu huingilia maovu kama vile ukahaba, wizi, kuasi wana, uchoyo na fitini kwa sababu ya uhitaji. Wengine wao huingilia maovu haya kwa sababu ya tamaa zao kubwa. King'ei anasema;

kila uchao twasoma, fulani kashikwa keba.
kote habari zavuma, vya watu kenda vibeba,
wajivunjia heshima, haba yajaza Kibaba
tamaa imewakaba, acheni milimbikizo.

King'ei alidhamiria kuonyesha namna tamaa ya mali inavyowafanya binadamu kukosa uhalisia wa maisha. Tamaa hii kulingana na mtumzi si kila kitu na haiwezi kuinunua furaha ya kweli ndipo anasema "Haba yajaza kibaba" anatumia methali hii kuhimiza kutosheka na kidogo mtu anachokipata kwa jasho lake kuliko kujiingiza katika maovu kwa kutaka vingi huku akiongozwa na tamaa.

Kwa umbuji wa mtunzi, kichwa cha shairi "Acheni milimbiko"ndicho kipande cha mkarara wa shairi lote. Aidha, ndicho kinachoongoza ujumbe wa shairi nzima.Mwandishi anakariri "Tamaa imewakaba" semi hii inadhihirisha kuwa tamaa ya mali imezidi na hivyo kuzidisha uovu. Vile vile, anasema kuwa "Kote habari zavuma''kwa maana ya kuenea kwa habari za wizi. Aonavyo mtunzi uovu kama huu anavyobainisha katika mshororo wa tatu hapo juu "Wajivunjia heshima". Semi hii inadhihirisha uovu huu unamfanya mtu kudharauliwa.

Aidha, mtunzi wetu anasema kuwa watu hawatulii nyumbani waume na wake "Daima wamo mbioni" kwa maana kuwa kila mara wanajishughulisha kutafuta mali. Anaendelea kusema kuwa, ndoa yao imekosa furaha na hata "Wameasi hata wana" kwa maana ya kutowajali na kuwalea wana kwa misingi dhabiti yenye maadili kwa sababu ya kutafuta mali. Anamaliza aya ya pili kwa kusema "Huu ni uhayawani" hii ni jazanda kwa ambavyo hayawani ni mnyama, katika muktadha huu anaona mienendo ya kutotosheka na mali hata kujingiza katika maovu ni kukosa adabu na utu.

King'ei anatuchorea taswira ya wanaume kwa wanawake wanaojizatiti kuimarisha maisha yao kwa njia mbalimbali. Wanawake kwa hivyo wameanza kukaidi ukubwa na utawala wa mwanaume katika mambo yote ya maisha. Mwanamke anaonekana kuanza

kushindana na mwanaume ili pia naye afaidi uhuru wa kiuchumi ndipo anasema "Leo Juma na Amina, hawatulii nyumbani"

Anaendelea kusema "Matumbo kama mapipa" tashibihi hii inadhihirisha kuwa wana pupa ya kutapia kila kitu bila kuwajali wenzao wasiokuwa nacho. Hii ndiyo sababu King'ei anasema "Choyo imewakalia" semi hii ina maana kuwa hawataki kuwapa wengine kitu chochote kwa ambavyo wana tabia ya kunyima hii imetokana na "Kwa kupenda kunenepa" hii ni jazada inayoonyesha tamaa ya kuwa na mali mengi.

Hali hii ya kutafuta mali ndiyo chanzo cha baadhi ya wasichana kushawishika kuuza miili yao ili kupata mali. Aidha, ndicho chanzo cha taasubi za kiume ambapo wanaume wanachukulia wanawake kama vifaa vya kujistarehesha mradi wametoa mali. Kwa hivyo, wanawake wamekuwa kama vyombo au vitu vya kununuliwa. Jambo hili linaonyesha kuwa maadili ya kijamii hayatiliwi maanani tena kwa sababu za kiuchumi. Ubinafsi na kule kujali mali ni vitu ambavyo vimevunjilia mbali utu. Rai hizi zinajitokeza katika ubeti wa sita ambapo King'ei anasema kuwa;

> nimeona siku nyingi, hasa hawa kina dada
> wayatenda mambo mengi, yasiyo ya kawaida.
> kutafuta mali mengi, na kutojali ya ada
> tuzingatie kaida, acheni milimbikizo

Katika aya hii, King'ei anatuonyesha namna tamaa ya mali inavyowakengeusha akina dada na wakawa na mtazamo hasi katika maisha na hasa kuhusiana na mali. Tamaa hii kwa hivyo ndiyo inayowafanya kukosa utu mwisho wakaathirika vibaya namna anavyoeleza katika mshororo wa pili na wa tatu "Wayatenda mambo mengi, yasiyo ya kawaida. Kutafuta mali mengi, na kutojali ya ada". Huu ndio uozo wa kiuchumi.

Aidha, anawatahadharisha watu juu ya tamaa ya mali mengi ambayo wamejilimbikizia. Anatoa mifano kuwa wanatafuta pato na mapesa yasiyo na idadi “Si vyakula si makao”. Takriri hii inasistiza jinsi watu walivyo na tamaa ya kujilimbikizia mali ya aina aina. Anatumia semi “Mwisho usijelemaa choyo ikawapofusha”kwa maana ya kuwa na tamaa nyingi na kukengeuka mwisho kukosa utu na kuwa mwenye tabia ya kuwanyima watu. Kwa kawaida kupofusha ni kufanya mtu asiweze kuona. Kwa hivyo mali kwa mujibu wa King’ei yaweza kumfanya mtu kukosa kuwadhamini wenzake wanaohitaji msaada wake. Anaendelea kusema kuwa mali ya wizi haifai kwa sababu ina laana na hivyo amependekeza “Ujitume kazi”. Hii ni semi yenye maana kuwa watu wafanye kazi kwa bidii hata kama ni duni “hata iwe ushairi”. Kwa ambavyo msanii huwa na dhamira ya kuandika yale yanayojenga jamii kimaadili. Hivyo basi kubainisha majukumu ya King’ei katika kuirekebisha jamii kimaadili.

Vilevile, anashangazwa na namna watu wamechukua mali kuwa kama dini kwa hivyo watu wanadhamini sana mali. Ndiyo sababu anasema “Kuabudu yetu mali” kwa maana ya kupenda mali kupita kiasi hivi kwamba wanajamii wanawavunjia wanajamii wengine heshima na hali kwa kuwafitini. Kwa kushadidia uovu huu anasema “Kufanya chini chini” hii ni semi yenye maana ya kutumia hila au ujanja na hata pia kutumia dawa za uganga “Uramali” ili kuleta madhara kwa wengine kwa minajili ya kupata mali. Maudhui haya yanajitokeza katika ubeti ufuatao.

yamekuwa ndiyo dini, kuabudu yetu mali.
wengine twawafitini, wavunjikiwa na hali.
kufanya kichini chini, hata pia uramali.
nasisitiza kauli, acheni milimbikizo.

King'ei anaendelea kushangazwa kwa namna watu wanajilimbikizia mali nyingi ndipo anasema"Vitu vingi kochokocho". Takriri hii inadhamiria kuonyesha vitu vingi wanavyojilimbikizia ili waweze kutukuka. Tamaa hii imezidi kwa ambavyo mtunzi anasema "Mwataka hiki na hicho" kwa maana ya bila kubagua wanachohitaji kwa hivyo anawahimiza binadamu waweze kujenga maadili kwa kusema "Utu msije utupa, kwa kula visivyolika". Hii ni jazanda kwa maana kuwa wasifanye uovu bali wafuate maadili yanayohitajika. Aidha anaendelea kuwahimiza washukuru na kutosheka kwa chochote wanachokipata kwa ambavyo ndivyo alivyoamuru "Mungu Mwumba Mtukuka" King'ei anataja majina tofautitofauti ya Mungu ili kusistiza ujenzi wa maadili yanayoambatana na dini.Kwa ambavyo umuhimu wa uadilifu ni kutovunja kiapo au kusaliti marafiki.

Katika shairi "Mbona matatu zaua" uk 157 lililo katika *Miale ya Uzalendo*. Anabaini uozo unaotokana na pesa miongoni mwa madereva wa matatu. Watu hawa wanaabudu pesa kuliko utu, hivyo kusababisha ajali, anaona kuwa usafiri kupitia kwa magari una hatari nyingi kwa ambavyo kuna mikasa inayowafika wanajamii. Mtunzi anasema "unapofunga safari" semi hii ina maana kuwa mtu anapoanza safari hukumbwa na hatari nyingi kwa ambavyo mwendo wa magari huwa wa kulegalega huku yamebeba watu na mzigo mingi kupita kiasi.

Kutowajibika kwa dereva wa matatu kunasababisha ajali nyingi kwa sababu dereva hao hawajali maisha ya abiria bali pesa mathalan;

> dereva wake jamani.
> katu hapati leseni.
> haja yake ni mapeni
> matatu mbona zaua?

Katika aya hii, King'ei anabainisha dereva kama wenye tamaa ya pesa kwa kuwa haja yake ni pesa bali si kuangalia maslahi ya abiria. Vilevile, tunamwona dereva huyu licha ya kuwa anaendesha matatu hajahitimu kwa ambavyo hana leseni. Anachotaka ni "Mapeni". Vilevile, mtunzi kwa kutumia swali la balagha "Matatu mbona zaua? Ni kejeli kwa dereva ambao wanasababisha maafa kwa wanajamii. Aidha, ndicho kibwagizo cha shairi hili, ili kusistiza maafa ya wanajamii yanayosababishwa na dereva wasiojali maisha.Vilevile, kibwagizo hiki ndicho kinachoongoza ujumbe wa shairi nzima.

Anaendelea kutuchorea taswira ya matatu zinazowaua wanajamii. Anasema kuwa matatu hizi zina vyuma vichakavu, vya darini na vya mbavu, na liendapo huwa si tulivu, matatu hizi zabeba sana na wala hazina hadhari huku viti vyake tunaviona vikibana. Aidha, matatu hizi zajaa watu huku vyuma vyake vikiwa na kutu. Licha ya magari haya kuwa mabovu ni kinaya kuwa yanabeba sana. Vilevile, mwendo wake huwa wa kasi "Kama upepo wa kusi" tashbihi hii ni kejeli kwa magari haya mabovu yanayoendeshwa kwa mwendo wa kasi kwa kulinganishwa na upepo wa kusi. Dereva wanapoendesha magari haya kwa mwendo wa kasi na kuyaacha yakiwa mabovu huku yakibeba sana, haja ya dereva hawa huwa ni tamaa ya pesa ili kujiinua kiuchumi. Anazidi kusema;

madereva hawajali
muradi wao ni mali
hawana katu kauli
matatu mbona zaua?

Kwa hivyo mtunzi wetu anashadidia ukosefu wa usalama katika sekta ya uchukuzi kwa kusema kuwa tunaposafiri "Moyo tumpe kahari" semi hii inaashiria kukosa matumaini ya kusafiri salama bila kuhusika kwenye ajali. Kwa hivyo, matumaini ya wasafiri kusafiri salama huwa kwa Mwenyezi Mungu ambaye anaongoza kila safari kwa kuwasitiri dhidi

ya ajali. Vilevile anakejeli, Dereva wa matatu kwa ambavyo "Huwa kalewa chakari" wanapoendesha matatu, hii inadhihirisha tamaa yao ya pesa. Aidha, tashbihi hii inadhihirisha kutojali maslahi ya abiria kwa ambavyo kiini cha ulevi huu ni kuzidisha machachari katika kuendesha matatu kwa nia ya kupata pesa nyingi. Hivyo basi King'ei anawahimiza madereva kujisaka na kujenga maadili yanayohitajika. Kwa mujibu wa nadharia ya maadili inayoshikilia kuwa sana ina uwezo wa kusimulia mambo yanayohusiana na maadili. Hivyo basi,kuona namna dereva wameendeleza uozo katika jamii.

Katika shairi "Walalahoi" uk36 lililo katika diwani ya *Wasakatonge.* Khatib anabainisha kundi la watu wachache wanaomiliki mali na nyenzo za usalishaji mali dhidi ya waliowengi. Mtunzi anachora taswira ya watu ambao wanafanya kazi kwa bidii katika ngazi mbalimbali za maisha hasa kazi za kijungu-jiko lakini hawafaidi jasho lao. Taswira hii inatokana na kunyanyaswa na kunyonywa na wenzao. Kwa kuandika shairi hili mtunzi anaonyesha kuwa unyonyaji huu unaongeza ufukura, mateso na unyonge kwa umma. Anasema;

makuli wa bandarini
wachuzi wa sokoni,
na wale mikokoteni
walalapo huwa hoi
fedha zao huwa duni
ni walalahoi.

Katika shairi hili, "Walalahoi" ni kichwa ambacho kimetumiwa kijazanda pia ndicho kinaongoza ujumbe wa shairi nzima. Khatib anaonyesha matatizo yanayowakumba wananchi kutokana na hali ngumu ya maisha. Anadhihirisha kuwa licha ya wao kufanya kazi za sulubu hadi wakachoka sana bado hawafaidi juhudi zao. Kwa ambavyo "Fedha

zao huwa duni" kwa maana ya thamani za pesa wanazopata baada ya kufanya kazi huwa ndogo au hafifu.

Aidha, anaendelea kusema kwamba wanaofanya kazi za ukulima, uwindaji, uchungaji wa mbuga Vilevile hulala wakiwa hawawezi kujimudu lakini manufaa au faida wanayopata baada ya kufanya kazi hizo haipo. Aidha, anaendelea kutaja wafanyakazi kama wachimbaji migodi, mafuta ardhini, wajengao maroshani, waashi, wavuvi, wamachinga, mafundi wa viwandani, manesi, manamba, wachuuzi sokoni, wasukuma mikokoteni miongoni mwa wafanyakazi wengine hawafaidi jasho lao. Hii ndiyo sababu mtunzi huyu anasema "Kipato hawakioni".

Khatib anasema kwamba, baadhi ya kazi hizi ni hatari kwa maisha ya wale wanazozifanya anatoa mifano ya kazi kama uchimbaji wa migodi na mafuta ardhini. Anasema kuwa wanaofanya kazi hizi "Roho zao mikononi". Semi hii ina maana kuwa kazi hizi ni hatari kwa ambavyo wafanyakazi hawa wanaweza kupoteza maisha yao wakati wowote. Pamoja na kupitia hatari hizi na kulala wakiwa wamechoka sana "Ziada hawaioni". Hii ni ishara kuwa wananyonywa na kunyanyaswa kwa kuzugwazugwa na kuamwa jasho lao kwa kuwa ni wanyonge.

Mwandishi kwa kuandika shairi hili alikuwa na dhamira ya kuangazia uozo wa kiuchumi unaoendelezwa katika jamii. Vilevile, kutuonyesha jinsi maudhui ya upotovu wa madili yanawiana na matumizi ya lugha. Kwa kufanya hivi, anawahimiza watu wajikwamue kiuchumi na kujiendeleza lazima waondoe miongoni mwao nyenzo za unyanyasaji. Nyenzo hizi ndizo zinazosababisha uozo wa kiuchumi. Aidha, watu lazima wajikinge dhidi ya vishawishi vya kuupunja uchumi. Kuna haja ya watu kuwa macho kujilinda

dhidi ya uvamizi wa uchumi miongoni mwao na nje kwa kufanya hivi watu lazima wajisahili wenyewe na kurekebisha matendo yao yenye uozo kwa manufaa ya umma kwa ambavyo sanaa ina uwezo wa kusimulia mambo yanayohusiana na maadili.

Khatib katika shairi "Klabu" uk 50 lililo katika diwani ya *Wasakatonge.* Anwani ya shairi hili imetumiwa kijazanda kwa kuonyesha namna dunia ilivyo na nchi zinazonyanyasa nchi zingine. Aidha, kichwa hiki ndicho kinachoongoza ujumbe katika shairi nzima

Katika ubeti wa kwanza mtunzi anatueleza kuwa alidhani ni klabu ya watu ambao ni wastaarabu na 'Walojaa adabu' ni semi yenye maana ya walio na matendo yenye heshima na staha. Ubeti wa pili ni kinaya cha ubeti wa kwanza kwa ambavyo si klabu ya usawa hivi kwamba 'Imejaa shakawa" semi yenye maana ya dhiki na masumbuko ambayo "dhamiriye kuuwa" kwa maana ya kutesa na kunyanyasa.

Kwa nchi ambayo ni maskini "Hujitia imani" kwa maana kuwa wanapokutana na nchi zilizoendelea huwapa mikopo. Mikopo hii huandamana na shindikizo na "Masharti mzomzo" ni takriri yenye maana ya masharti tele ambayo huambatana na vikwazo. Khatib anatueleza;

> kila wakutanapo,
> na mizengwe huepo,
> ya kutoa mikopo
> hutoa shindikizo,
> masharti mzomzo
> kuweka na vikwazo

Anaendelea kukariri kuwa,nchi hizi hukemea nchi maskini na hata kuambiwa mambo ya kuudhi kwa kuwakumbusha wema waliopata kuwafanyia waliopokuwa na shida. Aidha, huambia nchi nyingine mema waliowatendea nchi maskini walopokuwa na shida kwa

madhumuni ya kuwaaibisha huku nchi maskini "Twasujudiya" hii ni kejeli kwa ambavyo nchi maskini zimeenzi nchi zilizoendelea huku nchi hizi zikiendeleza dhuluma na mateso kwa nchi maskini. Kwa kuwaaibisha na kuwadhalalisha hivyo basi "Utu kufisha" semi yenye maana ya kuumbua ubinadamu kwa kuwadhalalisha.

Khatib anahimiza nchi maskini kuacha "Ombaomba". Takriri hii inasistiza nchi maskini kukoma kuhitaji misaada kutoka kwa nchi zilizoendelea. Aidha, anaendelea kusema kuwa nchi hizi sizitegemee nchi hizi "Ila tuchape kazi" kwa maana ya kutia bidii kwenye kazi kwa kutumia ujuzi wetu.

Aidha, anaendelea kusema kuwa wavijenge viwanda na "Kilimo kutanda" kwa maana ya kufanya kazi ya ukulima, vilevile, wawe wafugaji. Anahimiza kukuza uchumi na kujingatia elimu ndipo tusipoteze mapato yetu.

Khatib anapinga rushwa kwa kusema "Tupige vita rushwa" kwa maana ya kumaliza ufisadi kwa juhudi za kufanya kazi kwa bidii. Hivyo basi "Tutajenga heshima" kwa maana ya kupata hadhi ambayo walikuwa wameidhalalisha kwa kutiwa aibu. Kwa hivyo taifa litauwa imara na "Simango zitokoma" kwa maana ya kule kuaibishwa kutafika tamati

## 4.3 Kiishilio

Uhakiki wa mashairi ya uozo kiuchumi umeonyesha kwamba, watunzi wana mbinu zinazotumiwa kuibusha ujumbe wao. Watunzi wametumia mbinu ambazo zimesaidia kueleza na kutoa ujumbe wao ipasavyo. Wameangazia ugandamizaji na unyonyaji wa kiuchumi wa wanyonge, hivyo basi, kuwaathiri kwa kuwafanya kuwa watumwa na kuteseka huku wanaofaidi matunda ya kazi yao wanazotegeleza wanyonge ni wenye

nguvu. Baadhi ya mashairi yameangazia bara la Afrika kuwa wanyonge huku bara la Ulaya kuwa wenye nguvu za kiuchumi wao wanawagandamiza na kuwanyonya waafrika. hivyo basi watunzi wetu wanahimiza wenye nguvu za kiuchumi kujirekebisha na kujenga maadili yanayokubalika kwa mujibu wa nadharia ya maadili inayoshikilia kuwa umuhimu wa uadilifu ni kutovunja kiapo au kusaliti marafiki. Katika sura ya tano tumetoa muhtasari wa sura mbalimbali, matokeo ya utafiti, umuhimu, changamoto na mapendekezo ya utafiti zaidi.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

### 5.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia muhtasari wa sura mbalimbali. Aidha, tumeonyesha matokeo ya utafiti, umuhimu wake pamoja na kupendekeza maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

### 5.1 Muhtasari wa utafiti

Utafiti ulichunguza uozo katika mashairi ya Khatib na King'ei kijamii, kisiasa na kiuchumi katika diwani mbili; *Miale ya Uzalendo* (2000) na *wasakatonge* (2003). Malengo ya utafiti yalikuwa matano ambyo ni; kuonyesha namna mashairi yenye maudhui ya uozo ya Khatib na King'ei yanaathiri jimii. Aidha, kubaini namna uozo huo unavyoendelezwa. Isitoshe, kuonyesha wanaohusika katika kuendeleza uozo huo. Vilevile, kudhihirisha nafasi ya watunzi wetu wa mashairi katika kuirekebisha jamii na namna watunzi wa mashairi walivyoshughulikia suala la uozo katika mashairi yao.

Ukiukaji wa maadili katika jamii ni swala ibuka na nyeti, hivyo kulikuwa na umuhimu wa kulichunguza jambo hili katika jamii ya sasa ili kulielewa vilivyo kwa kuzingatia athari zake na jinsi ya kukabiliana nazo.

Uteuzi wa mashairi ulifanywa kwa njia ya kimaksudi kwa kuteua mashairi ishirini na moja yenye maudhui ya uozo, namna ya uendelezaji wa uozo huo, wanaohusika katika kuendeleza uozo, jinsi watunzi walivyoshughulikia suala la uozo na nafasi ya watunzi wetu katika kuirekebisha jamii.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Katika sura ya kwanza tumetanguliza kwa usuli wa utafiti. Vilevile, tumebainishadhima ya fasihi katika jamii na nafasi ya mtunzi kwa jamii anamoishi. Mbali na utangulizi tumeshughulikia suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, na sababu ya kuchangua mada. Aidha, tumebainisha upeo na mipaka ya utafiti ambapo tumetoa sababu ya kuwateua watunzi wetu.Isitoshe tumeshughulikia yaliyoandikwa kuhusu mada. Mbali na hayo, tumeonyesha misingi ya nadharia ambapo tumebainisha mihimiliya nadharia ya kimtindo na nadharia ya maadili. Vilevile, tuliweza kubainisha mbinu ya utafiti, muundo wa utafiti, pahala pa utafiti, sampuli lengwa na uteuzi wa sampuli, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo yetu ya utafiti.

Sura ya pili tumechanganua mashairi ya uozo wa kijamii kwa lengo la kumeonyesha uozo na namna uozo huu umeendelezwa katika jamii na adhari zake. Isitoshe, tumebaini wanaohusika katika kuendeleza uozo huo. Aidha, tumeonyesha jinsi watunzi walivyoshughulikia suala la uozo katika utunzi wao na jinsi watunzi hao wamewajibika katika kuirekebisha jamii kimaadili.

Sura ya tatu tumechanganua mashairi ya uozo kisiasa. Tumeshughulikia mashairi haya kwa lengo la kubainisha madhara yake kwa wanajamii. Aidha, tumeonyesha uozo na namna uozo wa kisiasa umeendelezwa katika jamii kwa mujibu wa mashairi ya Khatib na King'ei. Isitoshe, katika mashairi ya uozo wa kisiasa tumeonyesha wanaohusika katika kuendeleza uozo huo, jinsi watunzi hao walivyoshughulikia swala la uozo katika mashairi yao na kudhihirisha nafasi ya watunzi hao katika kuirekebisha jamii kisiasa ili kujenga maadili.

Sura ya nne tumechanganua mashairi ya uozo kiuchumi. Tumechanganua mashairi haya kwa lengo la kudhihirisha jinsi mashairi ya Khatib na King'ei yenye maudhui ya uozo kiuchumi yanavyoathiri jamii. Aidha, tumebainisha uozo wa kiuchumi na namna uozo huo unavyoendelezwa katika jamii. Vilevile, tumeonyesha wanaohusika katika kuendeleza uozo huo. Isitoshe tumeonyesha jinsi watunzi hao walivyoshughulikia suala la uozo kiuchumi na kubaini nafasi ya watunzi hao katika kuirekebisha jamii kimaadili.

**5.2 Matokeo ya utafiti**

Malengo yetu ya utafiti yalikuwa; kuonyesha namna uozo unaathiri jamii, kubainisha namna uozo unavyoendelezwa, kuonyesha wanaohusika katika kuendeleza uozo huo, kueleza namna watunzi walivyoshughulikia suala la uozo na nafasi ya watunzi hao katika kurekebisha jamii kimaadili. Katika kuafiki malengo yetu diwani za *Miale ya Uzalendo* (2000) na *Wasakatonge* (2003) zilitumiwa.

Katika kuelezea matokeo ya utafiti, tumebainisha kwamba haingewezekana kutenganisha malengo hayo. Kwa mfano katika kueleza aina ya uozo vilevile tumegusia wanaoendeleza uozo huo, madhara yake, jinsi walivyoushughulikia swala la uozo katika tungo zao, namna unavyoendelezwa na wajibu wa watunzi katika kurekebisha hali hiyo.

Katika sura ya pili uozo unaojitokeza ni; chuki, uaji, unajisi, ulawiti, ufisadi, wivu, ukeketaji, visirani, tamaa, ugomvi na utesi. Sura hii amewabainsisha; wafitini, wenye chuki, wauaji, wafisadi, mahakimu, madaktari, makarani kwenye ofisi, wapenzi, wakewenza, mke na mume katika ndoa, wenye matata, wenye kutakia wengine mabaya, wenye wivu, ngariba wanaotegeleza tohara kwa wanawake, jeshi, polisi, wanajisi na walawiti kama wanaoendeleza uozo huo.

Kwa kuangazia wafitini wameonyeshwa kuwa ni watu wenye maneno yanayoleta ugomvi uadui chuki na uchongezi baina ya wanajamii hivyo kusababisha hata vifo. Watu wenye chuki vilevile wameonyeshwa kama watu wasiokuwa na mapenzi kwa wenzao hivyo basi wana roho mbaya kwa wanajamii. wauaji wameangaziwa kama wanaowachinja watu kwa kutojali utu, hivyo jamii kuathirika kwa kusababishiwa vifo. Aidha, wake wenza wamebinika kama wenye wivu na wanaotendeana maovu kama vile kuoneana wivu, kuendeana kwa waganga, kutukanana kwa kuitana wachawi, kupokonyana bwana, kulaumiana, kufitiana, kubomoleana nyumba, chuki miongoni mwa maovu mengine.

Watunzi wanapendekeza kuepuka maovu kama vile ufitini, matata, kujiingiza kwenye lawama,visirani, tamaa na chuki. Wanawashauri kutochekana na kuvunjiana heshima. Jamii iepuke vitisho  na kugombana katika uneni hata mawazoni, hivyo basi, kuacha chuki na kuondoa wivu kwa kuwa utengano una shari tupu.

Kupitia baadhi ya mashairi imebainika kuwa ufisadi umeenea kila pembe barani Afrika. Mahakimu katika mahakama hutoa hukumu yao kwa upendeleo kwa kuegemea rushwa. Aidha, madaktari, makarani kwenye ofisi, wapenzi vilevile wameangaziwa kama wenye kuendeleza ufisadi kwa kuwa sharti huduma zao ziweze kufisidiwa ndipo anayejihitaji azipate, hivyo basi jamii kukosa kupata haki na kuduma wanazopaswa kupewa.

Mume na mke katika ndoa vilevile wameangaziwa kama wanaotetana kwa kutusiana nakuchukiana. Wanagombana kwa sababu ya kukosa pesa za kukithi mahitaji kama vile chakula na karo ya watoto shuleni. Aidha, kwa kukosa kupatana kunasababisha kupigana na hivyo kusababisha hasara.Vilevile, utesi na chuki katika ndoa husababisha kutopiga hatua za kimaendeleo nchini na hivyo kudumu katika dhiki na kuwa kama

wanyama.Watunzi kwa kurekebisha jamii wanawashauri kukutana kwa kuwa haifai chochote kutetana na kuchukiana kwa sababu utengano ni adui.

Ngariba vilevile ameonyeshwa kama anayeendeleza uozo katika jamii. Kwa sababu amebainika kuwa anakeketa uke wa mwanamke bila hata tiba ya kutibu vidonda wanavyovisababisha. Hivyo basi, kusababisha maafa kwa wanajamii. Aidha, mazingira wanayotegelezea tohara huwa chafu, hutumia kiwembe kichafu na kibutu hivyo basi husababisha maradhi ya vidonda kama vile pepopunda. Mwanamke anapokuwa na hedhi vidonda hivyo huchangia uke wake kuvunda. Hutumia wembe mmoja kwa wari wengi hivyo basi kuambukizana ugonjwa wa ukimwi. Mtunzi huyu wanahimiza kuacha mila dhaifu ambazo zinawatesa na kuwaangamiza wanajamii vilevile anawazindua kukwepa amali chafu na hivyo kushika uadilifu.

Katika sura ya tatu mashairi ya uozo kisiasa yamechanganuliwa. Khatib na King'ei wamewamulika viongozi ambao ni marais, wabunge, mawaziri na viongozi katika taasisi mbalimbali ni viongozi mamlakani ambao wanaendeleleza uozo. Jamii ikiwa na matarajio kuwa wangeongozwa kwa mienendo yenye maadili kinyume chake viongozi hawa hawajawajibika. Wao wamesawiriwa kama wanaoendeleza uozo wa; ubinafsi, usaliti, tamaa, ubaguzi, chuki unafiki na udikteta.

Khatib anawaangazia viongozi hasa marais kama vile Bokasa, Idi, Mobutu kama marais madikteta ambao wanajidai kuwa wana nguvu ambazo hazitaisha milele kwa kuwalinganisha na "mungu watu." Uongozi wao mbaya unaangaziwa kama unaotumia risasi, mizinga na mitutu kuwagandamiza watu.

Aidha, viongozi wameonyeshwa kama wenye ubinafsi, hivi kwamba wanajilimbikizia mali huku umma ukihangaika kwa umaskini, umma unakandamizwa kwa kuwa wao ni wajakazi, wapagazi, washenzi, watwana na watumwa. Kwa kuwa viongozi wameleta usultani, ukoloni na uzayuni kwa hivyo utawala huu unatumia nguvu kunyanyasa raia.

Viongozi wanasababishia raia mahangaiko kwa maongozi yasiyofaa. Viongozi wanasozania uongozi na hivyo kusababisha kuzembea katika nyadhfa zao kwa kutowajibika kwa kutenda haki. Hivyo basi, raia wanaoongozwa kutaabika kwa kusalitiwa hasa wakongwe, akina mama na watoto. Watunzi wanaufahamisha umma uwe macho kwa kuangazia maovu ya viongozi wao ili waweze kuona tofauti iliopo kati yao na watawala wao. Wanawakabili viongozi wasio na utu hivyo kupinga unafiki wa viongozi wasiopenda kukosolewa. Vilevile wanaona dunia kama uwanja wa mapambano kati ya mabwana wachache na watwana wengi. Wanapendekeza njia ya pekee ya kuleta usawa ni kpitia mapinduzi jinsi inavyojitokeza katika shairi "Hatukubali".

Aidha,wamerejelea viongozi wanafiki na vigeugeu. Ambao wana tamaa ya kutaka kujinufaisha huku umma ukikosa kuthaminiwa ilhali wanajidai kuwa wao ndio wazalendo wakuu hivyo basi umma unawachwa katika lindi la umaskini. Mbali na hayo wamerejelea katiba ambayo haijali utu wala haki, yenye ukatili na ujangili, isiyofuata sheria ila hongo, katiba ya wenye shibe inayotetea tawala za mabavu badala ya katiba kuwafaa wananchi wote inawafaa wachache ambacho ni kinyume cha uadilifu hivyo basi viongozi wanaendeleza raha zao kwa kutumia jasho la raia.

Watunzi wanapendekeza katiba inayojali utu na haki, inayoondoa ujinga, kuondoa utawala wa mabavu, unafiki na ufisadi, isiyo ya wachache wateule, inayoondoa utabaka na ukoloni mamboleo.

Khatib anawatumia wanyama kijazanda kurejelea viongozi wanaojitukuza na kujitenga na umma na kuutawala kiimla, wenye mamlaka kugandamiza wanyonge kwa sheria zisizojali umma huku King'ei anakashifu ukoloni mamboleo. Viongozi wamesaliti uhuru uliopiganiwa na wananchi kwa kujitenga na kuwasahau wananchi wao badala yake wanashirikiana na mfumo wa kinyonyaji wa ukoloni mamboleo kuzidi kuwanyonya na kuwagandamiza wananchi wa tabaka la chini, wanadhulumiwa, kunyonywa, kuonewa kudharauliwa.Watunzi wanakashifu ukoloni mamboleo katika mataifa huru ya Afrika. Kwa kuwa ni hatari kwa ustawi wan chi yoyote ile. Kwa hivyo, suluhisho ni kukomesha mfumo huo uliojaa dhuluma, maonevu, kudharauliwa, kukandamizwa kwa waafrika.

Katika sura ya nne mashairi ya uozo kiuchumi yamechanganuliwa. Khatib na King'ei wamebainisha unyonyaji na umwaji wa jasho la wanyonge kwa manufaa ya wenye nguvu. Wanaoendeleza uozo huu ni bara la Ulaya dhidi ya bara la Afrika, dereva na wadau wengine wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali.

Tumeona kuwa bara la Ulaya linawagandamiza na kuwanyonya waafrika kwenye bara la Afrika katika nyanja zote si umma si serekali na hivyo waafrika kuwa matesoni kwa kuwa wanapangiwa mipango, kutolewa amri, pia wanapewa maagizona hata sera zote kuletwa Afrika. Vilevile, bara la Ulaya linatumia hila kuwazugazuga wanyonge na kuamwa jasho lao. Hali hii ya ubinafsi inavunja hali ya kiutu. Kwa kuangazia uozo huu

Khatib anawahimiza wanaohusika kukoma kuwagandamiza waafrika kwa kuwa ni uonevu.

Aidha wamebainisha tamaa ya mali ambayo husababisha wanajamii kuingilia maovu kama vile ukahaba, wizi, kuasi wana, uchoyo na ufitini. Ubinafsina kule kujali mali ni vitu ambavyo vimevunjilia mbali utu, hata hivyo mtunzi anapendekeza watu kufanya kazi kwa bidii.

Shairi "Mbona matatu zaua?" limebaini uozo unaotokana na pesa miongoni mwa dereva wa matatu, kwa hivyo wanaabudu pesa kuliko utu hivyo kusababisha ajali. Hawajali kupata leseni hivyo basi hawajahitimu na huendesha magari kwa mwendo wa kasi na kubeba sana kwa hivyo wanasababisha vifo. King'ei anapendekeza dereva kujali maslahi ya abiria, waweze kuhitimu kwa kupata leseni, kuyakarabati magari yao na kupunguza mwendo wanapoyaendesha magari hayo.

Watunzi wamebainisha kunyanyaswa na kunyonywa kwa wafanya kazi wa kijangu-jiko ambao hawafaidi jasho lao. Unyonyaji huu unaongeza ufukara, mateso na unyonge kwa umma. Baadhi ya kazi kama vile uchimbaji wa migodi na mafuta ardhini ni hatari kwa sababu wafanyakazi wanaweza kupoteza maisha yao wakati wowote. Kwa jumla watunzi wanapendekeza kuwa, nyenzo za uzalishaji mali zimilikiwe na kila mwanajamii bali si wanajamii wachache, hivi itaboresha maisha ya jamii yote kwa ujumla.

Tumetumia nadharia mbili katika kutimiza malengo yetu. Nadharia iliyoongoza utafiti huo ilikuwa nadharia ya kimtindo. Iliweza kuteuliwa kwa ambavyo inashikilia kuwa fasihi haiwezi kueleweka bila lugha. Kwa hivyo jinsi mtunzi atumiavyo lugha husaidia

kutoa ujumbe wake kwa wasomaji au wasikilizaji. Hivyo basi kazi ya fasihi hudumu kupitia mtindo wake na mtindo huo ni mtu mwenyewe.

Kwa mujibu wa muhimili wa kwanza maudhui na dhamira hushughulikia maoni au falsafa ya mtunzi juu ya jamii anayoizungumzia. Khatib na King'ei wameweza kuwa na dhamira ya kuadilisha na kueleza jinsi maudhui hayo ya uozo yanawiana na matumizi ya lugha wameweza kutumia jazanda, taswira, tashhisi, maswali ya balagha, takriri, semi, tashbihi.

Hata hivyo kupitia mhimili wa pili muundo wa kazi ya kubuni ndio hutumiwa na msanii kutoa ujumbe wake. Huu ni mkondo anaofuata msanii katika kuifuma kazi yake. Kwa mfano, jinsi mtunzi alivyounganisha tukio moja na lingine, wazo na lingine au ubeti na ubeti ama mstari na ubeti mwingine.Tuliposoma mashairi ya Khatib na King'ei imebainika kuwa watunzi walirudiarudia baadhi ya maneno katika mishororo ili kusistiza ujumbe wanaotoa. Aidha, watunzi wametumia maswali ya balagha katika mishororo ili kuibua mawazo na hisia za wasomaji kutafakari pamoja na mtunzi, baadhi ya vibwagizo ni vifupi. Aidha, watunzi wetu waliweza kuyagawa mashairi yao katika vipande mbalimbali vya mishororo.

Isitoshe tulitumia nadharia ya maadili inayomhusisha mwanafalsafa Plato anayeshikilia kuwa umuhimu wa uadilifu ni kutovunja kiapo au kusaliti marafiki. Aidha,sanaa ina uwezo wa kusimulia mambo yanayohusiana na maadili. Vilevile, msanii huwa na dhamira ya kuandika yale yanayojenga jamii kimaadili mwisho fasihi inaeleweka vyema inapohusishwa na mazingira ya kijamii.

Mhimili wa kwanza umeonyesha umuhimu wa kutovunja kiapo kwa marafiki. Ni bayana kuwa binadamu katika ngazi mbalimbali kama vile mahakimu, askari, madereva, marais, mawaziri, wabunge, wakewenza, wenye nyenzo za uzalishaji mali, dereva, wafitini, wenye chuki, ngariba, makarani ni baadhi ya wanajamii walioangaziwa katika mashairi ya uozo ya Khatib na King'ei. Wamevunja kiapo cha uaminifu kwa kutowajibikia majukumu yao ipasavyo.

Katika mhimili wa pili sanaa ina uwezo wa kusimulia mambo yanayohusiana na maadili. Kwa kuchanganua mashairi ya uozo katika diwani za mashairi ya Khatib na King'ei,wanawafahamisha jamii kuhusu uozo unaotukia katika jamii wanamoishi. Lengo lao kuu likiwa kuboresha na kuimarisha maisha ya jamii kama vizazi vya sasa na vya kesho. Haya ni mambo yanayowaathiri moja kwa moja. Kwa ambavyo fasihi inaelemweka vyema inapohusishwana mazingira ya jamii.

Kwa jumla utafiti huu umepata kuwa nadharia hizi zimesaidia katika kuangalia uozo katika jamii na namna ya kukabiliana nao. Kwa kuwa mtindo wa mwandishi huathiri uibushaji wa ujumbe wake.

## 5.3 Umuhimu wa matokeo ya utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu wa kuirekebisha, kuiongoza, kuielimisha na kuzindua jamii hasa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Utafiti huu umedhamiria kuwaandaa binadamu kuwa raia wema na waadilifu.

Aidha, unaweza kutumika kukabiliana na maswala nyeti yanayoathiri jamii yetu. Zaidi ya hayo utafiti umewadhihirishia wanajamii aina mbalimbali ya uozo ambao binadmu wamepitia na jinsi ya kukabiliana na uovu huo.

Aidha, umeweza kuonyesha nyufa zilizomo katika nyadhifa za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Dhamira yake ikiwa kuwakosoa na kuwaelekeza wanajamii kwa njia faafu.

**5.4 Mapendekezo**

Utafiti huu ulidhamiria kuonyesha namna Khatib na King'ei walivyowasilisha maudhui ya uozo katika mashairi yao kijamii, kiuchumi na kisiasa, utafiti mwingine unaweza kufanywa katika mashairi yenye maudhui tofauti.

Utafiti zaidi unaweza kuhusisha jinsi waandishi wa hadithi fupi, riwaya na hata tamthilia walivyoshughulikia suala la uozo.

Katika utafiti huu tumeshughulikia uwasilishaji wa uozo katika mashairi ya Khatib na King'ei, ambapo King'ei ni mtunzi kutoka Kenya ilhali Khatib ni mtunzi kutoka Tanzania.Tumebainisha kuwa watunzi hawa japo wametoka katika mazingira tofauti wameweza kuangazia swala la uozo kijamii, kiuchumi na kisiasa.Tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe kubainisha namna wanavyotofautiana katika kuyashughulikia maswala mbalimbali kwa kuegemea tofauti za kimazingira.

**MAREJELEO.**


Abdalla, A (1973) *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press

Abdalla na Sengo (1975) *Mlika* 7 Tanzania, Chuo Kikuu Dar Es Salaam Abedi, K.A (1958) Sheria Za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri. Nairobi: Kenya Literature Bureau

Ahmad Nassir (1971) *Malenga wa Mvita*. Nairobi: Oxford University Press

Amana, B. (1982) *Malenga wa Vumba*. Nairobi, Dar es Salaam: Oxford University Press

Benard, G. (2004) *Common Morality, Deciding what to do*. New York: Oxford University Press

Barkhressa, K. S. (2010). *Kamusi ya Maana Na Matumizi.* Nairobi: Oxford University Press

Chacha, M.C.(1987) *TheMeaning and Interpretation of Swahili Poetry*. Phd Thesis Yale University.

Chiraghdin, S. (1971) *Utangulizi wa Malenga wa Mvita*. Nairobi: Oxford University Press

_____________ (1986) *Malenga wa Mrima*. Dar es Salaam: Oxford University Press

Gibbe ,AG na Masoko DL W (1978) *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.*Dar es Salaam: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam

Gibbe, AG (1980) *Ushairi wa Shaban Robert*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House

Gicuru M (2007)*Usawiri wa Maudhuya Ndao Katika Ushairi wa Euphrase Kezilahabbi na Kithaka wa Mberia*. Nairobi: M A Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Greenblatt S (1980) *Rennaissance Self Fashioning*. Chicago: Univesity of Chicago




KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Greenblatt, S. na Gallegherc (2002) *Practising New Historicism*. Chicago: Univesity of Chicago

Fischer, E. (1959) *The Necessity of Art A Marxist Approach*. Middlesex: Penguin Books

Foucault ,M. (1979) *Discipline and Punish Translation ofSurveiller Et*, Punir Vintage.

______________ (2002) *The Archaeology of Knowledge Trans AM Sheridan Smith*. London and New York: Routledge.

James, B. R. (2006) *The Telegraph Business Club Leader*. London: Hodder Arnord Great Britain London Bath Press Ltd

J. S Mdee, na E. Mbogo (1985) *Mlika* 17. Taasisi ya Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili. Tanzania: Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam.

Johnson, F (1985) *Kamusi ya Kiswahili*. London: Oxford University Press Kezilahabi, E. (1974) Kichomi. Nairobi: Heinman Education Books.

Kibwana, K. (1996) *Sowing the Constitutional Seed in Kenya*. Nairobi: Claire Press. Kimani

King'ei, K. (2002) *Miale ya Uzalendo*. Nairobi: Phonex Publishers.

King'ei, K. na Kemoli A. (2001). *Taaluma a Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers

Leech, G. (1969) *A Linguistic Guid to English Poetry*. New York: Longman Group Uk Ltd

Lunacharsky, A. (1965) (Ed 1973). *On Literature and Art*. Moscow: Progress Publishers

Masamba, D.P.B (1976) *Diwani ya Masamba*. Nelson: EA

Msokile, M. (1994) *Miongozo ya Lugha na Fasihi na 5, Uchambuzi Na Uhakiki Wa Ushairi.* Dar Es Salaam: Dar Es Salaam Univerty Press.

Masinde, E. W (1992) *Ushairi Huru; Uchambuzi wa Dhamira Na Mtindo*, Tasnifu ya M A Nairobi: Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

________( 2003), *Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo Na Mabadiliko ya Maudhui*, Phd Nairobi: Chua Kikuu Cha Kenyatta.

Mlacha, S. A. K. (1984) *Riwayaza Visiwani* (1970- 1980)na Ujenzi wa Jamii Mpya Katika Mlika na 16. Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam. TUKl

Mnyampala, M. (1980) *Johari za Kiswahili Na 5*. Diwani Ya Mnyampala Dar es Salaam: East Africa Bureau

Mungathia Robert (2011) *Ufumbaji Wa Mashauru Ya Kiswahili. Mfano Wa Malenga Wa Mvita Na Malenga wa Vumba*. M A Nairobi: Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.

Njogu (2007) *Governance and Development towards Quality Leadership in Kenya.* Nairobi: Twaweza Communication Ltd 23

_________(1997). *Uhakiki wa Riwaya la Visiwani Zanzibar*. Nairobi; Nairobi University Press.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nyamaume, A.K. (1976) *Diwaniya Ustadhi Nyamaume*. Nairobi: Shungwa Publishers Ltd Stanford Encyclopedie of Philosophy (2004)

Sengo, T. (1977) *Shaban Roberty Uhakiki wa Maandishi Yake*. Longman East Africa

Senkoro, F.M.K. (1988) *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

_______________(1988) Ushairi :Nadharia na Tahakiki

Tolstoy, L. N. (1960). *What Is Art Translated By AlmyerMande*. New York: Macmillan

Wamitila, K.W (2002) *Uhakiki wa Fasihi*, Misingi na Vipenge/e Vyake. Nairobi: Phonex Publishers

Wafula,R. M. Na K. Njogu (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wa Thiong'o, Ngugi, (1981). *Writers in Politics*. Nairobi: General Printers Ltd.

FAHARASA

**Kiambatisho I: Maelezo ya istilahi muhimu kama zilivyotumiwa katika tasnifu**

1. **UOZO :-**Kupotoka kimaaadili ambapo matendo na mienendo ya mtu huwa mibaya.
2. **UOZO WA KIJAMII** :- kupotoka kwa maadili yanayohusu watu wengine, maswala na malengo ya jamii nzima kama vile ndoa, dini, mapenzi na falsafa za kijamii.
3. **UOZO WA KISIASA :-** ni ile tabia hasi ya viongozi wa kisiasa katika mamlaka. Anavyoingiliana na washindani na vile uongozi huo unavyotegemea na watu wa jamii kama ilivyoathiri hapo awali, sasa na hata baadaye.
4. **UOZO WA KIUCHUMI**: - kupotoka kimaadili ambapo msingi wake ni kuwa kila mwanajamii hawezi kutambua uwezo wake wa kuzalisha mali kwa ambavyo anagandamizwa.
5. **TASWIRA-** Taswira ni mkusanyiko wa picha mbalimbali zinazoundwa kutokana na maelezo ya mwandishi. Taswira hutoa picha ya vitu au mandhari ya mahali kupitia ishara zinazomfanya msomaji kupata miguso mbalimbali. Kwa hivyo jukumu la taswira ni kuweza kujenga dhana katika akili na kusaidia kuumba na kuangaza uhalisi wa mambo ya jamii.
6. **METHALI-** Methali ni usemi wa kifalsafa wenye maneno maalum yasiyobadilika na ambayo yamezoeleka katika jamii na hupokezwa kutoka kizazi hadi kizazi hutumiwa kulinganisha hali mbalimbali za maisha katika jamii methali imetumiwa kudhihaki na kuupa uhai ushairi zaidi.

7. **TASHIBIHI-** Hii ni tamathali ya usemi ambapo watu au vitu viwili au zaidi hulinganishwa na watu au vitu kwa kutumia maneno: kama vile, mithili ya, kama, kama kwamba, mfano wa na kadhalika. Katika tasnifu hii, Tashbihi imetumiwa kupanua, kuyakinisha na kuupa uhai ushairi zaidi.

8. **TASHIHISI-** Katika tamathali hii, kitu kusichokuwa na sifa walizonazo viumbe wenye uhai hupewa sifa hizo. Hivyo basi katika ushairi huu imetumiwa kuzindua akili ya msomaji na kuyapa uhai mashairi.

9. **BALAGHA-** Balagha ni matumizi ya maswali ambayo hayahitaji majibu ya moja kwa moja. Majibu ya maswali haya hutarajiwa kufahamika au kueleweka na msikilizaji au hadhira. Yametumiwa kusisimua na kuchoma moyo na kuchochea huzuni, chuki na hata mzinduko wa msomaji.

10. **TAKRIRI-** Haya ni marudio kwenye sentensi au semi ambayo nia yake huwa ni kusistiza. Mtindo huu umetumiwa ili kufanya jambo linalozungumziwa kumwingia msomaji moyoni na kulielewa vyema.

**11. TABAINI-** Katika aina hii ya tamathali, mwandishi husistiza jambo fulani kupitia mtindo wa kinyume. Msisitizo huu hufanyia kwa kutumia neno "si" la kukanusha. Katika ushairi huu tabaini imetumiwa kuzindua akili ya msomaji alidhibiti vizuri jambo linalozungumziwa.

**12. KEJELI-** Ni usemi wa majumbo ambao maneno yake huwa ya dhihaka, hata kudharau hivi kwamba hutoa wasifu wa matendo yasiyofaa ilhali ana maana ya kinyume chake. Katika kazi hii kejeli imetumiwa kwa kuwazindua wasomaji kuangazia maovu wanayotenda binadamu.

13. **SITIARI-** Ni tamathali ya usemi ambayo kitu matendo au vitu vyenye hulka mbalimbali hulinganishwa na hali sawasawa na maumbile au jinsi ya utendaji.

14. **KINAYA-** Ni usemi wa kimafumbo ambao maneno yake huwa kinyume fulani katika usemi, hali au tukio, hivi kwamba utokeaji wa jambo unakwenda kinyume na matarajio ya msomaji au mhusika anayepatikana katika kazi fulani.

**Kiambatisho II: Mashairi Teule**

i) **MASHAIRI YENYE MAUDHUI YA UOZO YA KITULA KING'EI**
**Diwani ya Miale ya Uzalendo (2000).**

1. **Wafrika unganeni.**

Bara letu, Afrika
Muda wetu umefika
Mapinduzi kufanyika
Na silaha kuzishika
Hadhi yetu kutetea.

Kwa dahari na dahari
Bara letu la fahari
Metukalia bepari
Adui wenye ghururi
Weusi kutuonea.

Utumwani tumedumu
Maisha yenye ugumu
Watunyoya yetu damu
Na huku wala vitamu
Mali zetu watwalia.

Watu wetu wameuzwa
Ugenini kuingizwa
Masulubu kufanyizwa
Utu wao kupuuzwa
Adui kuhudumia.

Miyaka mingi ilipitia
Ndugu zetu wakitweta
Kupigana vingi vita
Vya uhuru kuupata
Waweze kuendelea.

Nchi zetu wakazivuja
Sina haja kuwataja
Siku nyingi metupuja
Bara letu kukalia.

Walitumia mabavu
Kutukalia kwa nguvu
Kufanyia maovu
Dhuluma na maonevu
Masilahi kulindia.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Wazalendo 'liungana
Wakoloni kupigana
Mikono walishikana
Misaada kupeana
Mapambano kuchachia.

Pigano lilipochacha
Madola waliyaacha
Enzi mpya ilikucha
Ikachorwa mpya picha
Weusi kutawalia.

Mkoloni 'liondoka
Ingawa hakutoweka
Bara letu Afrika
Ukoloni waoneka
Pembe nyingi angalia.

Afrika ya Kusini
Weusi wamo tabuni
Wanaishi hatarini
Katu hawana amani
Kaburu kuwaonea.

Waishi kwa ubaguzi
Nyumbani na kwenye kazi
Wadunishwa waziwazi
Kwa majonzi na machozi
Kila hali waumia.

Wauliwa kila siku
Hawaishi dukuduku
Mahali huko na huku
Wateseka kila siku
Weupe kutumika.

Namibia vile vile
Mambo ndiyo yale yale
Ukoloni mambo-kale
Popote nchini mle
Ndiyo watumwa sikia.

Ilo baki kwa hakika
Ni silaha kuzishika

Kuilinda Afrika
Hadhi yetu kuiweka
Uhuru kupigania.

Weupe wametutesa
Mafani wametutosa
Kuokoka kwetu sasa
Ni kupigana hususa
Afrika kukomboa.

Kukomboa Afrika
Juhudi yahitajika
Isiwe ni patashika
Dada zangu hata kaka
Afrika tuungane.

**2. Uvundo**

Nenda mjini hata kijijini
Ingia zahatini ama hospitalini
Ndwele yako mwilini, hupati afuweni
Kisa? " Mkono mtupu..."

Nenda maofisini, ingiahata mahakamani
Uwe mashitakani ama tuseme umo malamikoni
Maneno ya kilingeni, utafikiri punguani
Kisa? Dua la mnyonge..."

Nenda kizimbani usimame hukumuni
Kijitoa "hatiani", katu huwezi asilani
Ukibaki ujingani, usizunguke mbuyuni
Kisa, "Mti hauendi..."

Nenda maofisi, ukatafute makarani
Kwamba u taabani huduma waitamani
Neno moja abadani, hutapata la maani
Kisa, "Mtaka cha mvunguni..."

Nenda ukumbini, mahojiano kazini
Maswali yote wabaini, majibu yote kughani
Umefaulu yakini, bali kazi wakuhini
Kisa, "Damu nzito..."

Nenda barabarani, kwamba u safarini
Hata uwe matembezini, hapo kwenu jirani
Watukutia mbaroni, nia mbovu wakudhani
Kisa, "kuku wa maskini..."

Nenda hapo mtaani, kuzurure madukani
Mara hapo kundini, chokora kanyakua jani
Watakuponda kichwani, kumtia mautini
Kisa, "Aso na bahati…"

Nenda makutanoni, wakutanapo fulani
Iwe ni karamuni, wakaapo mezani
Mijizi na mihuni, itawekwa namba wani
Kisa, "Ni nusu ya shari…"
Nenda matembezini, uingie mahabani
Mapenzi ya moyoni, yakuzonge akilini
Iwapo hamna kibindoni, hudhaminiwa asilani
Kisa, Bunduki bila risasi…"

Nenda kote nchini, tembea bara na pwani
Maovu wayatamani, wema autambua nani?
Ni kauli ya duniani, ametuonya maanani
Fisadi haiwezekani, yavunda bila ubani.

3. **Kinyume cha katiba**
Hatuitaki katu
Katiba yenye idhilali
Isotambua watu
Katiba yenye ukatili
Isokuza utu
Katiba ya ujangili

Katiba ya kutuaza njaa
Yenye kutulisha jaani
Katiba ya wenye shibe
Na unasi kuangamia
Katiba yatufaani
Iwapo twaangamia?

Katiba iso haki
Haki ya wenye nacho
Katiba iso sheria
Sheriaze ni mfuko
Katiba ya kuzunguka mbuyu
Pasina njia ikawepo

Katiba ya uchaguzi
Uchaguzi wa uteuzi
Achaguliwaye siye
Ateuliwaye ndiye
Apendwaye tumchukie
Achukiwaye tumpende
Hii ndiyo katiba?

**4. Wake wenza**

BIBI 1
Bibi mdogo nakuonya
Waniona kama nyanya
Unazidi kuninyonya
Nyumba wanifilisia

BIBI 2
Bi mkuwa wachukiza
Kila siku wanapiza
Uadui kuukuza
Kwa nini wanifatia?

BIBI 1
Tabia zako si nzuri
Kiburi umekithiri
Pia nyingi taksiri
Ambazo wanifanyia.

Kila siku nakariri
Kukuonya acha shari
Wazidisha na fahari
Pasipo kunisikia.

BIBI 2
Uwache chako kiwewe
Ubaya watenda wewe
Yafaa ulaumiwe
Maovu kunitendea.

Ni mtu mnyenyekevu
Wala sina hata wivu
Si mtumiaji nguvu
Vipi wanilaumia?

BIBI 1
Huishi kwenda pembeni
Na kule vichochoroni
Na wale wako wandani
Maneno kunitilia.

Wanidai ni mchawi
Pamoja na mengi mawi
Unayasema hayawi
Ingawa wanitakia.

BIBI 2

Kusengenyana sijui
Wala hata hakufia
Bali nyumbani hukai
Kila siku wakimbia.

Wanisema sina nguo
Na uvumi kama huo
Na wala huna kituo
Ukakaa kutulia.

BIBI 1

Kinachoniudhi sana
Ni kunipokonya bwana
Liye nizalia wana
Kwako umemfungia.

Mi naye umetutenga
Kwa madawa kumzinga
Uelewe zako kunga
Kitambo nafahamia.

BIBI 2

Usemayo ni muhali
Nayaona bure ghali
Si maneno ya halali
Bure wajiropokea.

Bwana sikukupokonya
Kilimi ninakukanya
Mapenzi hujayafanya
Mmeo kumfanyia.

BIBI 1

Mapenzi unayotaja
Kuwa nayo sina haja
Siku nyingi nimengoja
Bwanangu kunirudia.

Ni madawa wamlisha
Na nyingi sana bashasha
Ili kumbabaisha
Ndivyo unavyotumia.

BIBI 2 Ni bure wanishitaki
Lawama zisizo haki
Unyumba hauuweki
Bwanayo kumwangalia.

Mapenzi ukimwonyesha
Kicheko kumchekesha
Chini utamketisha
Hapo kwako kutulia.

BIBI 1 Wanionea kijicho
Wewe mkavu wa macho
Sijui unitakacho
Nyumba kunibomolea.

Ilivyokuwa twaishi
Bila moja tashiwishi
Nawe kijicho huishi
Kutwa wanifatilia.

BIBI 2 Kwa nini unapotoka
Ama kusema hakika
Nyumba sote twaiweka
Bwana ni wetu sawia.

Ninayosema sikiza
Raha zetu wakatiza
Ndiye aliyeningiza
Humu nyumbani sikia.

BIBI 1 Najua wanidharau
Bali hili sisahau
Nakuomba angalau
Heshima kuniwekea.

Mwenyewe unatambua
Jukumu nilichukua
Na ukae ukijua
Mi wa mwanzo kuingia.

BIBI 2 Lau wataka heshima
Yapime unayosema
Umwogope na Karima
Aliyeumba dunia.

Jamii ilo imara
Ukumbuke kila mara
Inahitaji stara
Heshima nzuri kutia.

**5. UZUZU**

Mbele yenu nimejiri, kauli yangu kusema
Nataka kuwahubiri, jambo linaloniuma
Sitaki liwe ni siri, lijulikane na umaa
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Wakati wa ukoloni, wakenya tuliungana
Tulijitia vitani, si wazee wala wana
Tukafanya juu chini, kila hali kukazana
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Tulipotwaa hatamu, kujitawala nchini
Tukaliacha jukumu, tuliloshika mbeleni
Ikatungua hamu, ilotujaa moyoni
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Tukajitwalia viti, alivyoacha Mzungu
Madaraka si katiti, yakagawanywa mafungu
Walokuwa na bahati, wakachwewa na ukungu
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Wongozi tuliposhika, katia nyingi nadhiri
Tukawa tuna hakika, kumaliza ufakiri
Zikapita hekaheka, lakini bila ya ari
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Adui wetu ujinga, bado hajatwondokea
Japo twazidi kupanga, njia hijatunyokea
Shabaha tuliyolenga, yataka kujitolea
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Walopata uongozi, baadhi walilegea
Ikawa mali kuozi, tama kuwakolea
Wakaidharau kazi, kwa pato kulizegea
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Usitawi huzorota, kwa kutopata mwongozo
Umma hasara hupata, nchi hujazia uozo
Siku huja na kupita, vyeo huviza mawazo
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Adui wapya sikia, wametokeza bayana
Sasa nitawatajia, tupate kuelewana
Wa kwanza aloingia, ni sisi kutopatana
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Hasa walo kwenye vyeo, wakawa watubagua
Kwa kufikia upeo, wengine kutowajua
Ikawa ni kila leo, wapendapo kujizuzua
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Wakasahau ukweli, cheo huwa ni dhamana
Wakajitenga kwa mbali, tukakosa kuonana
Sote tukawa ni tuli, bila moja kufaana
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Ikawa ni kutengana, kukaweko matabaka
Kila siku kupigana, kuwekeana mipaka
Badala ya kupendana, tukaishi kama kaka
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Tama zetu na chuki, ndiyo adui wa pili
Wenye vyeo hawataki, walo chini kukabili
Wanafanya taharuki, kuwaka ja pilipili
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Waloketi kwenye viti, wakawa watukumbusha
Zamu moja hampati, ingawaje mwatutisha
Mngatumia na chati, bure mwajitaabisha
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Huko mlioko chini, bakieni huko huko
Nguo tieni rahani, jingine lenu haliko
Mwafikiri akilini, tutajarudi mliko
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Wa tatu adui wetu, ni kutothamini kazi
Japo uwezo ni wetu, na tumeipanda ngazi
Hakika baadhi yetu, tumeshindwa waziwazi
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Kwamba tumejitawala, yatupasa kukumbuka
Tufanyize halahala, nchi ipate kujengeka
Isiwe kunywa na kula, matumbo mbele kuweka
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Vyeo tulivyovishika, kwa kung'oa mkoloni
Yatupasa kuviweka, ili kujenga watani
Haifai kuzuzuka, kuwa kama hayawani
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

Hadi hapa nasimama, nanyi mpate fikiri
Yote niliyoyasema, na pia kuyakariri
Inafaa kuyapima, ili kuepuka shari
Uwezo na utukufu, visituzuzue jama.

**6. Mbona Mwateta**

Wenzangu mawteteani, kucha kutwa mitaani
Mkaapo majumbani, na hata vichochoroni
Kiwasumbuacho nini, hebu nifahamisheni
Nawaomba mpatane, utengano ni adui.

Daima mwasumbuana, na chuki kufanyiana
Mabaya mwatakiana, kutwa mwalaumiana
Fitina mwatiliana, bayana kutukanana
Nawaomba mpatane, utengano ni adui.

Mke na mume nyumbani, nanyi mwagombea nini
Mwakosa pesa 'fukoni, au chakula tumboni
Watoto nao shuleni, tulieni masomoni
Nawaomba mpatane, utengano ni adui.

Kila mnapopigana, na hasara kutiana
Mnazidi kutengana, kwa kukosa kupatana
Kwa nini mnavutana, mnapaswa kupendana
Nawaomba mpatane, utengano ni adui.

Mkumbuke asilani, hatutasongea nchini
Iwapo hatupatani, tutadumu taabani
Tutakuwa hayawani, tutembeapo njiani
Nawaomba mpatane, utengano ni adui.

Kwa nini mnakosana, maovu kuapizana
Vijembe mwatiliana, na wivu kuoneana
Heri kusaidiana, baada ya kushindana
Nawaomba mpatane, utengano ni adui.

Tuepuke visirani, tumalize ufitini
Tusingie matatani, tujitoe lawamani
Haifai kutamani, chake Ali na Hassani
Nawaomba mpatane, utengano ni adui.

Kwa wazee na kwa wana, tujaribu kupatana
Tuache kuoneana, na masinzi kupakana
Tusiwe wa kuchekana, heshima kuvunjiana
Nawaomba mpatane, utengano ni adui.

Tusikazane uneni, na mawazo akilini
Vitisho tuviacheni, tuoneane imani
Chuki tuiweke chini, na wivu tuondoeni
Nawaomba mpatane, utengano ni adui.

Hasara mnaziona, wala faida hapana
Haifai kutetana, au kamwe kutengana
Tujaribu kukutana, mashauri kupeana
Nawaomba mpatane, utengano ni adui.

### 7. Acheni Milimbiko

Kusimulia naanza, jambo lililo nisibu
Nawaulizeni kwanza, ili mpate nijibu
Ni nani aliyeanza, wengine kutuadhibu
Naona mwajighilibu, acheni milimbikizo.

Leo Juma na Amina, hawatulii nyumbani
Furaha pia hawana, daima wamo mbioni
Wameasi hata wana, wamejituma chumoni
Huu ni uhayawani, acheni milimbikizo.

Naye Njoroge na Mbuka, nyumbani mwao wateta
Akiba nyigi kuweka, ili kwepuka matata
Shida mtu kutosheka, ama amani kupata
Maisha jama yapita, acheni milimbikizo.

Wenzagu acheni pupa, kila kitu kutapia
Matumbo kama mapipa, kwa matonge kubugia
Kwa kupenda kunenepa, vya wenzenu mwajilia
Choyo imewakalia, acheni milimbikizo.

Baadhi wanajihini, ndipo wapate lundika
Wafikiri akilini, kwamba watatjirika
Eti siku za mbeleni, waje kuwa watukuka
Amekataza Rabuka, acheni milimbikizo.

Nimeona siku nyingi, hasa hawa kina dada
Wayatenda mambo mengi, yasiyo ya kawaida
Kutafuta mali mengi, na kutojali ya ada
Tuzingatie kaida, acheni milimbikizo.

Wazee ndo pia nao, siku hizi wamezidi
Kutafuta pato lao, mapesa yaso idadi
Si vyakula si makao, wavishika kama gudi
Maovu mmeshitadi, acheni milimbikizo.

Na vijana ndio hasa, wamezidi wasiwasi
Kuzegea nyingi pesa, kujiwekea ukwasi
Kumi karibu na tisa, hazitatosha fulusi
Vipi mwazidi uasi, acheni milimbikizo.

Kila uchao twasoma, Fulani kashikwa keba
Kote habari zavuma, vya watu kenda vibeba
Wajivunjia heshima, haba yajaza kibaba
Tama imewakaba, acheni milimbikizo.

Nchini kumeienea, harakati kila fani
Kina unapotembea, nyumbani au kazini
Vioja tajionea, vya pupa kutamani
Mnalimbika vya nini, acheni milimbikizo.

Ukizoa ushukuru, kupata kuna Rabuka
Ndivyo alivyoamuri, Mungu Mwumba Mtukuka
Tusifanye kukufuru, hasara itatufika
Yachukiza kwa hakika, acheni milimbikizo.

Kulundika vilimwengu, kwa kutaka kusifiwa
Huzusha mengi machungu, kunafaa kukimbiwa
Si ya leo ni ya tangu, kama tulivyousiwa
Mtakuja vunjikiwa, acheni milimbikizo.

Kila nifikiriapo, sioni haja yake
Mtu kutoka alipo, kwenda kula vya wenzake
Neleze yake malipo, nelewe natija yake
Mbona mwafanya makeke, acheni milimbikizo.

Chanzo chake ni tamaa, mali mengi kuzalisha
Kwa mtu alokomaa, yafaa kujiepusha
Mwisho usije lemaa, choyo ikakupofusha
Malizeni mshawasha, acheni milimbikizo.

Mali katu hayawezi, nafsi kutusitiri
Hasa mapato ya wizi, yamejawa na ghururi
Bora ujitume kazi, hata iwe ushairi
Shikeni langu shauri, acheni milimbikizo.

Yamekuwa ndiyo dini, kuabudu yetu mali
Wengine twawafitini, wavunjikiwa na hali
Kufanya kichini chini, hata pia uramali
Nasisitiza kauli, acheni milimbikizo.

Ni kipi mkitakacho, katika zenu nafsi
Vitu vingi kochokocho, ili mpate anisi
Mwataka hiki na hicho, mwazidisha wasiwasi
Msikiuke viasi, acheni milimbikizo
Kaditamati ni hapa, wala mbele sitafika
Mawaidha nimewapa, ili mpate uongoka
Utu msije utupa, kwa kula visivolika
Enyi shangazi na kaka, acheni milimbikizo.

**8. Ndumakuwili**

Kuuma na kuvuviza, kaziye ndumakuwili
Tabiaye ukiwaza, mpuzi hana kauli
Uhasama hutukuza, ni mwongo na bahili
Hakika ndumakuwili, ni adui wa jamii.

Kiongozi bila sera, kama chombo baharini
Kila mtu humkera, hana analobaini
Hurukaruka ja chura, hupati yake kanuni
Hakika ndumakuwili, ni adui wa jamii.

Muhali kuaminika, bana mbele wala nyuma
Atendayo yana shaka, hasa unapoyapima
Huzama na kuibuka, hatui ila kuhama
Hakika ndumakuwili, ni adui wa jamii.

Kugombanisha wenzake, kaziye ndumakuwili
Kuhami kilicho chake, kiwe hali au mali
Si mume wala si mke, ndumakuwili bahili
Hakika ndumakuwili, ni adui wa jamii.

Mathalani atasema, "Fulani huyu ni nyani"
Tena 'tatoa lawama, " mwenzako kakwita nyani"
Sipogundua mapema, hutoweza kumlani
Hakika ndumakuwili, ni adui jamii.

Yakini hana rafiki, ndumakuwili fahamu
Ndumakuwili nafiki, nyendo zake ni haramu
Mazaoye nyingi chuki, na uwongo wa kudumu
Hakika ndumakuwili, ni adui wa jamii.

Ndumakuwili mfano, kiongozi ofisini
Kujitakia vinono, wenzake kutothamini
Huyakenua meno, "mzalendo namba wani"
Hakika ndumakuwili, ni adui wa jamii.

Ndumakuwili kanisani, misikitini daima
Sababuye madhumuni, matilabaye kuchuma
Kumbe yaliyo moyoni ni uozo ukipima
Hakika ndumakuwili, ni adui wa jamii.

Kinywa chake ni ladhati, kiwa katika hadhira
"Hana ubaya katiti", kimtazama kwa sura
Ndumakuwili mufti, kuzua yake madhara
Hakika ndumakuwili, ni adui wa jamii.

Ndumakuwili nakoma, sifaze kusimulia
Sipomfeli mapema, hasarani utangia
Inafaa kumpima, kila analokwambia
Hakika ndumakuwili, ni adui wa jamii.

**9. Mbona Matatu Zaua?**

Mkasa umetufika
Ni janga kuu hakika
Jama wetu waponzeka
Matatu mbona zaua?

Unapofunga safari
Kusafiri kwa magari
Ni nyingi zake hatari
Matatu mbona zaua?

Mwendo wake wa kupwaya
Labeba haya na haya
Mwenzetu nazicheleya
Matatu mbona zaua?

Dereva wake jamani
Katu hapati leseni
Haja yake ni mapeni
Matatu mbona zaua?

Anapoendesha gari
Huwa kalewa chakari
Huzidisha machachari
Matatu mbona zaua?

Vyuma vyake vichakavu
Vya darini na vya mbavu
Lendapo si tulivu
Matatu mbona zaua?

Matatu zabeba sana
Wala hadhari hazina
Viti vyake vya kubana
Matatu mbona zaua?

Mwendo wake ni wa kasi
Kama upepo wa kusi
Zaenda bila kiasi
Matatu mbona zaua?

Madereva hawajali
Muradi wao ni mali
Hawana katu kauli
Matatu mbona zaua?

Tuabiripo matatu
Ambazo zajaa watu
Vyuma vyote vina kutu
Matatu mbona zaua?

Iwapo tunasafiri
Moyo tumpe kahari
Pekee atusitiri
Matatu mbona zaua?

Matatu hapa kikomo
Na mimi mwenzenu nimo
Nataka kwenda kagumo
Japo matatu zaua.

**10. Afrika Yaugua**

Bara letu Afrika
Lateseka kwa hakika
Kwa madhila kaka kaka
Yalofika Afrika.

Zimetimu heka heka
Ukombozi kuusaka
Roho nyingi kututoka
Za wana wa Afrika

Sasa vita vimefuka
Kila pembe Afrika
Kote bunduki zalika
Kuitweza Afrika.

Mama yetu Afrika
Wanao tutateseka
Kwa majanga kutufika
Wana wako Afrika.

Maisha yetu yatutoka
Ni tama kujitwika
Mkoloni atucheka
Kukucheka Afrika.

Ufiisadi umewaka
Mzomo tunataka
Akiba mzozo kuweka
Kufisidi Afrika.

Wana wako Afrika
Utu wetu watutoka
Uadui watukuka
Kati yetu wafrika.

Chuki yetu inawaka
Ndugu na ndugu kupoka
Visasi vingi kuweka
Kwangamiza Afrika.

Bara letu langulika
Ndani yake linalika
Ni maradhi kulishika
Kwambukiza Afrika

Ufukara Afrika
Kote kote unawake
Bara zima kuliteka
Fukarisha Afrika.

Mauaji Afrika
Kila pembe yatapaka
Siasa zetu tupoka
Huru wetu Afrika.

Wana wako Afrika
Kilio kinawatoka
Kulilia Afrika
Bara letu Afrika.

**ii) MASHAIRI YENYE MAUDHUI YA UOZO YA KHATIB DIWANI YA WASAKATONGE**

**1. TOHARA**

Tohara, kwa mwanamke, ni hatari,
Madhara, kwa wake uke, hushamiri,
Hasara, yap eke yake, hudhihiri,
*Zinduka!*
Epuka, hao ngaroba, wajuaji,
Hufika, navyo viroba, wachinjaji,
Kumbuka, hawana tiba, wauaji,
*Amka!*
Kiwembe, kilochafuka, na kibutu,
Viumbe, huathirika, ni kwa kutu,
Siombe, yakakufika, mwana kwetu,
*Zinduka!*
Maradhi, hujitokeza, ya vidonda,
Yaridhi, kujichomoza, pepopunda,
Na hedhi, hukuchagiza, ikavunda
*Amka!*
Isiwe, wembe mmoja, wengi wari,
Ujuwe, ukimwi huja, ni hatari,
Na iwe, katu si hoja, kuwa mwari,
*Zinduka!*
Mzazi, kujifunguwa, idhilali,
Huwezi, kujitanuwa, ni muhali,
Ni wazi, husumbuliwa, na misuli,
*Amka!*
Wacheni, mila dhaifu, zinotesa,
Kwepeni, amali chafu, nawaasa,
Shikeni, uadilifu, tangu sasa,
*Zinduka!*

**2. AFRIKA**

*Lini?*
Afrika utakuwa,
*Bustani ya amani,*
Ukabila kuuzika,

Udini kuufyeka,
*Ni lini?*
*Lini?*
Afrika utakuwa,
*Ziwa la utulivu,*
Kufisha uonevu,
Kumaliza uovu,
*Ni lini?*
*Lini?*
Afrika utakuwa,
*Takia la upendo,*
Kujenga uzalendo,
Wenye uzuri mwendo,
*Ni lini?*
*Lini?*
Afrika utakuwa,
*Tamati ya fitina,*
Kuacha kuchinjana,
Kuanza kupatana,
*Ni lini?*
*Lini?*
Afrika utakuwa,
*Radi yenye chereko,*
Nderemo na vicheko,
Raha iso mashiko,
*Ni lini?*
*Lini?*
Afrika utakuwa,
*Bwawa la utajiri,*
Kufuta ufakiri,
Hali iwe nzuri,
*Ni lini?*
*Lini?*
Afrika utakuwa,
*Kitalu chenye shibe,*
Na njaa isikabe,
Pia watu washibe,
*Ni lini?*
*Lini?*
Afrika utakuwa,
*Sayari ya uzima,*
Kupata siha njema,
Magonjwa kuyazima,
*Ni lini?*
*Lini?*

Afrika iutakuwa,
*Adui wa ukame,*
Kwa yoyote uhame,
Na usikuandame,
*Ni lini?*
*Lini?*
Afrika utakuwa,
*Nongwa ya mafuriko,*
Yanoleta vituko,
Pia mahangaiko,
*Ni lini?*
*Lini?*
Afrika utakuwa,
*Bikira wa uhuru,*
Nema iwe vururu,
Pasiwe la kudhuru,
*Ni lini?*
*Lini?*
Afrika utakuwa,
*Ni pepo ya dunia,*
Raha kuogeleya,
Dhiki kuzikimbiya,
*Ni lini?*

### 3. HATUNA KAULI

Hatuna sisi kauli,
Ni kwa yetu maduhuli,
*Si umma si serikali.*
Mavuno yetu shambani,
Na dawa nazo mashini,
*Ulaya bei ni duni.*
Vitu vyao viwandani,
Na dawa pia mashini,
*Bei zake za thamani.*
Maagizo tunapewa,
Mipango tunapangiwa,
*Na amri tunatolewa.*
Sera zote siyo zetu,
Zimeletwa huku kwetu,
*Hazina faida katu.*
Twapewa yake mitaji,
Tuwe wasimamiaji,
*Pia watekelezaji.*
Zatumika nguvu zetu,



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Bila yakupata kitu,
*Chenye na faida kwetu.*
Hakika ni uonevu,
Kwa kujifanya werevu,
*Wenye mbinu na mabavu.*

**4. MADIKTETA**

Madikteta
   Katika,
   Dunia hii ya tatu,
   Na hasa Afrika yetu,
Itele "Mungu watu"
Bokasa, Idi, Mobutu,
Mizinga nayo mitutu,
Haitoi risasi,
Hutoa maraisi,
Walio madikteta,

**5. MIAMBA**

*Ingawa* umenuna, ishavu vyako kutuna,
Kunapambazuka, jua linatoka,
Bado kunakucha,
      *Kwa heri.*
*Ingawa* menisusia, kujipa kunigomeya,
Mvua zanyesha, masika hukesha,
Hakuna ukame,
      *Kwa heri*
*Ingawa* menivimbia, hutonipasukiya,
Kujaa na kupwa, bahari hukupwa,
Hatufuriki,
      *Kwa heri.*

**6. HATUKUBALI**

*Hatukubali tena,*
Kuja tena ili kuonewa,
Kuja tena na kutawaliwa,
Hatukubali katu,
Ndani ya nchi yetu,
*Iliyo huru.*
*Hatukubali tena,*
Kugeuzwa kuwa wajakazi,
Kugeuzwa kuwa wapagazi,
Kugeuzwa kuwa ni washenzi,

Ndani ya nchi yetu,
*Iliyo huru.*
*Hatukubali tena,*
Kwetu kuurejesha ubwana,
Kwetu kuurejesha utwana,
Kwetu kuurejesha utumwa,
Hatukubali katu,
*Iliyo huru.*
*Hatukubali tena,*
Kutuletea usultani,
Kutuletea na ukoloni,
Kutuletea na uzayuni,
Hatukubali katu,
Ndani ya nchi yetu,
*Iliyo huru.*
*Hatukubali tena,*
Kama wapo watu kama hao,
Na wavifunge virago vyao,
Wawafatiye mabwana zao,
Hatukubali katu,
Ndani ya nchi yetu,
*Iliyo huru.*
*Hatukubali tena,*
Tunakula kiapo kulinda,
Ya mapinduzi yetu matunda,
Tunakula kiapo kushinda,
Hatukubali katu,
Ndani ya nchi yetu,
*Iliyo huru.*

**7. MTEMEA MATE MBINGU**

Nimeona maajabu, mambo yaliyotendeka,
Nikashindwa kuwa bubu, kaamua kutamka,
*Tena bila ya aibu, maovu yalifanyika.*

Mate juu hayalengwi, jelezi napokushika,
Ingawa mtu hafungwi, kutema unapotaka,
*Kwa jambo hilo hafungwi, uso wako kuchafuka.*

Huchafua uso wake, sana ukaharibika,
Ikesha haiba yake, heshima kumalizika,
*Akatusi utu wake, asijue pakushika.*

Kutemea mate mbingu, na uso ukainuka,
Nakutumia mizungu, na mikakati kuweka,
*Hayavuki hata wingu, chini yataporomoka.*

Hata nguvu kitumiya, pale yanapomtoka,
Mate yatamrejeya, usoni tamgubika,
*Harufu kumwingiya, na wajihi ukanuka.*

**8. WALALAHOI**

Makuli wa bandarini,
Wachuzi wa sokoni,
Na wale mikokoteni,
Walalpo huwa hoi,
Fedha zao huwa duni,
*Ni walalahoi.*
Wakulima mashambani,
Wawindaji mawindoni,
Wachungaji wa mbugani,
Walalapo huwa hoi,
Masilahi hawaoni,
*Ni walalahoi.*
Wachimbaji migodini,
Na mafuta aridhini,
Roho zao mikononi,
Walalapo huwa hoi,
Ziada hawaioni,
*Ni walalahoi.*
Wajengao maroshani,
Waashi kuwa kazini,
Kwa nyumba zenye thamani,
Walalapo huwa hoi,
Malipo hayalingani,
*Ni walalahoi.*
Wavuvi wa baharini,
Wamachinga majiani,
Wapikao magengeni,
Walalapo huwa hoi,
Kipato hawakioni,
*Ni walalahoi.*
Mafundi wa viwandani,
Manesi hospitalini,
Na manamba mashambani,
Walalpo huwa hoi,
Pesa si matumaini,
*Ni walalahoi.*

### 9. WAFADHILIWA

Wafadhili kufurahishwa,
Ni sera zao kupitishwa,
Rais anaamrishwa,
*Tekeleza!*
Mawaziri wanajulishwa,
Sheria zinabadilishwa,
Na bungeni kuhalalishwa,
*Pitisheni!*
Ni sera za kunakamishwa,
Umma wote kuatilishwa,
Shida na dhiki kuvalishwa,
*Taabani!*
Taifa linadhalilishwa,
Mambo mengi kushurutishwa,
Na bila kushirikishwa,
*Yaoneni!*
Uhuru wetu twauuza,
Na heshima tunapoteza,
Historia itatubeza,
*Amkeni!*

### 10. NAHODHA

*Nahodha,*
Wang'ang'ania sukani,
Mechafuka, bahari siyo shuwari,
Si shuwari, pepo zinatuathiri,
Zaathiri, na mawimbi ni hatari,
Ni hatari, tufani meshamiri,
Meshamiri, na mvua zitiriri,
Zitiriri, radi nazo sikadiri,
*Nahodha tosa nanga!*

*Nahodha,*
Wang'ang'ania sukani,
Na jahazi, lenda mramamrama,
Mrama, na kupasuka mataruma,
Mataruma, mkuku umeachama,
Meachama, tanga limo kudatama,
Kudatama, foromali yainama,
Yainama, chombo sasa kitazama,
*Nahodha tosa nanga!*

*Nahodha,*
Wang'ang'ania sukani,
Abiria, sote tunateseka,
Teseka, kulewa na kutapika,
Kutapika, na ngama inatutoka,
Inatutoka, vikongwe vyasulubika,
Sulubika, mama wanayayatika,
Yayatika, vitoto vyataabika,
*Nahodha tosa nanga!*

*Nahodha,*
Wang'ang'ania sukani,
Tuendako, hatufiki si salama,
Si salama, sarahange alalama,
Alalama, abiria watetema,
Watetema, roho zao zaangama,
Zaangama, na mali zitayoyoma,
Zayoyoma, dhoruba metusakama,
Zasakama, utazibeba lawama,
*Nahodha tosa nanga!*

### 11. UNYAMA
Unyama wa binadamu,
Haukadiriki,
Haufikiriki,
Hausadikiki,
*Ni mnyama wa wanyama.*
Binadamu dikiteta,
Na nchi huzitawala,
Utawala wa kiimla,
Kwa mbinu na kwa hila,
*Ni mkandamizaji.*
Binadamu ana vyombo,
Amejenga mahakama,
Polisi chungu nzima,
Na jeshi la kuandama,
*Kuadhibu "wakaidi"*
Binadamu ni mlafi,
Hula vya baharini,
Nyama zote porini,
Na mazao shambani
*Hata ndege warukao.*
Binadamu mwangamizi,
Huunda silaha kwa siri,
Silaha zilizo hatari,

Umma zitazowaathiri,
*Dunia kuangamia.*
Binadamu hana aibu,
Ni kawaida kubaka,
Wasichana kunajisi,
Wavulana kulawiti,
*Mufilisi wa maadili.*
Binadamu mmiliki,
Anayafuga majini,
Kuyatumia mashetani,
Kuongea mizimuni,
*Na kuwadhuru wengine.*
Binadamu hawezekani,
Huamka na kulala,
Hufika kila mahali,
Dunia kuitawala,
*Hata mwezini kafika.*
Binadamu hatosheki,
Hivi sasa yu tayari,
Anatafuta sayari,
Aitimize dhamiri,
*Kuendeleza unyama.*

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY